# Mambo Ya Walawi

*Sadaka ya kuteketezwa*

1 Mwenyezi Mungu akamwita Musa na kusema
naye kutoka Hema la Kukutania, akamwambia,
2 “Sema na Waisraeli, uwaambie, ‘Yeyote mion-
goni mwenu anayeleta sadaka kwa Mwenyezi
Mungu, alete mnyama kama sadaka yake kutoka
kundi lake la ng’ombe, au la kondoo na mbuzi.
3 “ ‘Ikiwa sadaka hiyo ni sadaka ya kuteketezwa
kutoka kundi la ng’ombe, atamtoa ng’ombe dume
asiye na dosari. Ni lazima amlete kwenye ingilio
la Hema la Kukutania ili aweze kukubalika kwa
Mwenyezi Mungu.
4 Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha
sadaka ya kuteketezwa, nayo itakubaliwa kwa
niaba yake ili kufanya upatanisho kwa ajili yake.
5 Atamchinja yule fahali mchanga mbele za
Mwenyezi Mungu, kisha wana wa Haruni walio
makuhani wataleta damu na kuinyunyiza pande
zote za madhabahu yaliyo penye ingilio la Hema
la Kukutania.
6 Ataichuna hiyo sadaka ya kuteketezwa na
kuikata vipande vipande.
7 Wana wa Haruni kuhani wataweka moto juu
ya madhabahu na kupanga kuni juu ya huo moto.
8 Kisha hao wana wa Haruni walio makuhani
watapanga vile vipande vya nyama, pamoja na
kichwa na mafuta ya huyo mnyama, juu ya zile
kuni zinazowaka juu ya madhabahu.

9 Ataziosha sehemu za ndani za yule mnyama
pamoja na miguu yake kwa maji; naye kuhani atavichoma vyote juu ya madhabahu. Hii ni sadaka ya kuteketezwa, sadaka iliyotolewa kwa moto, yenye harufu nzuri ya kumpendeza Mwenyezi Mungu.

10 " 'Ikiwa sadaka ni sadaka ya kuteketezwa
kutoka kundi la kondoo au mbuzi, atamtoa dume asiye na dosari.
11 Atamchinjia upande wa kaskazini wa mad-
habahu mbele za Mwenyezi Mungu, nao wana wa Haruni walio makuhani watanyunyizia damu yake pande zote za madhabahu.
12 Atamkata vipande vipande, naye kuhani
atavipanga, pamoja na kichwa na mafuta ya mnyama juu ya zile kuni zinazowaka juu ya madhabahu.
13 Ataosha sehemu za ndani na miguu kwa
maji, naye kuhani atavileta vyote na kuvichoma juu ya madhabahu. Hii ni sadaka ya kuteketezwa, sadaka iliyotolewa kwa moto, harufu nzuri ya kumpendeza Mwenyezi Mungu.

14 " 'Ikiwa sadaka inayotolewa kwa Mwenyezi
Mungu ni sadaka ya kuteketezwa ya ndege, atamtoa hua au kinda la njiwa.
15 Kuhani atamleta kwenye madhabahu, naye
atamvunja shingo na kumnyofoa kichwa na kumchoma juu ya madhabahu. Damu yake itachuruzishwa ubavuni mwa madhabahu.
16 Ataondoa kifuko cha chakula pamoja na
uchafu wake na kuvitupa upande wa mashariki wa madhabahu, mahali pale penye majivu.

17 Atampasua na kumweka wazi katika
mabawa yake, lakini asimwachanishe kabisa,
kisha kuhani ataichoma juu ya zile kuni
zinazowaka juu ya madhabahu. Hii ni sadaka
ya kuteketezwa, sadaka iliyotolewa kwa moto,
harufu nzuri ya kumpendeza Mwenyezi Mungu.

# 2

*Sadaka ya nafaka*

1 “ ‘Mtu yeyote aletapo sadaka ya nafaka kwa
Mwenyezi Mungu, sadaka yake itakuwa ya unga
laini. Atamimina mafuta juu yake, aweke
uvumba juu yake,
2 naye atapeleka kwa makuhani wana wa
Haruni. Kuhani atachukua konzi moja unga
laini na mafuta, pamoja na uvumba wote, na
kuviteketeza kama sehemu ya kumbukumbu juu
ya madhabahu, sadaka iliyotolewa kwa moto,
harufu nzuri ya kumpendeza Mwenyezi Mungu.
3 Sadaka ya nafaka iliyobaki ni ya Haruni na
wanawe; ni sehemu ya sadaka iliyo takatifu sana
iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto.

4 “ ‘Kama utaleta sadaka ya nafaka iliyookwa,
itakuwa ya unga laini: iwe maandazi yaliyoten-
genezwa bila kutiwa chachu, yaliyochanganywa
na mafuta, au mikate myembamba iliyoten-
genezwa bila kutiwa chachu na iliyopakwa
mafuta.
5 Iwapo sadaka yako ya nafaka imeandaliwa
kwenye kikaango, itakuwa ni ya unga laini
uliochanganywa na mafuta, bila chachu.

6 Vunjavunja na kumimina mafuta juu yake; hii
ni sadaka ya nafaka.

7 Ikiwa sadaka yako ya nafaka imepikwa
kwenye sufuria, itatengenezwa kwa unga laini
na mafuta.

8 Ilete hiyo sadaka ya nafaka iliyotengenezwa
kwa vitu hivi kwa Mwenyezi Mungu; mkabidhi
kuhani, ambaye ataipeleka madhabahuni.

9 Naye atatoa ile sehemu ya kumbukumbu
katika hiyo sadaka ya nafaka, na kuiteketeza
juu ya madhabahu kuwa sadaka iliyotolewa kwa
moto, harufu nzuri ya kumpendeza Mwenyezi
Mungu.

10 Sadaka ya nafaka iliyobaki ni ya Haruni na
wanawe; ni sehemu ya sadaka takatifu sana kati
ya sadaka zilizotolewa kwa Mwenyezi Mungu
kwa moto.

11 " 'Kila sadaka ya nafaka unayoleta kwa
Mwenyezi Mungu ni lazima ifanywe bila ku-
tiwa chachu, kwa kuwa huna ruhusa kuchoma
chachu yoyote au asali katika sadaka inay-
otolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto.

12 Unaweza kuzileta kwa Mwenyezi Mungu
kuwa sadaka ya malimbuko, lakini haziwezi ku-
tolewa juu ya madhabahu kama harufu nzuri ya
kupendeza.

13 Koleza sadaka zako zote za nafaka kwa
chumvi. Usiache kuweka chumvi ya agano la
Mungu wako katika sadaka zako za nafaka; weka
chumvi kwenye sadaka zako zote.

14 " 'Ukileta malimbuko ya sadaka ya nafaka
kwa Mwenyezi Mungu, utatoa masuke yaliyo-
pondwa ya nafaka mpya iliyookwa kwa moto.

15 Weka mafuta na uvumba juu yake; ni sadaka
ya nafaka.
16 Kuhani atateketeza ile sehemu ya kum-
bukumbu katika hiyo sadaka ya nafaka iliyo-
pondwa, na mafuta, pamoja na uvumba wote,
kuwa sadaka iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu
kwa moto.

# 3

### *Sadaka ya amani*

1 " 'Ikiwa mtu anatoa sadaka ya amani, naye
akatoa ng'ombe, akiwa dume au jike, atamleta
mnyama asiye na dosari mbele za Mwenyezi
Mungu.
2 Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha
sadaka yake na kumchinja penye ingilio la Hema
la Kukutania. Ndipo makuhani, wana wa Haruni,
watanyunyiza damu ya huyo mnyama pande
zote za madhabahu.
3 Katika hiyo sadaka ya amani ataleta sadaka
iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto:
sehemu za ndani na mafuta yote yanayoungana
nazo,
4 figo zote pamoja na mafuta yaliyozifunika
karibu na kiuno, na kipande kirefu cha ini;
utayaondoa pamoja na figo.
5 Kisha wana wa Haruni wataiteketeza juu ya
madhabahu, juu ya ile sadaka ya kuteketezwa
iliyo juu ya kuni zinazowaka; ni sadaka ya
kuteketezwa kwa moto, harufu nzuri ya kumpen-
deza Mwenyezi Mungu.

6 “ ‘Akitoa kondoo au mbuzi kutoka kundi kuwa
sadaka ya amani kwa Mwenyezi Mungu, atamtoa
dume au jike asiye na dosari.
7 Akimtoa mwana-kondoo, atamleta mbele za
Mwenyezi Mungu.
8 Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha
sadaka yake, naye atamchinja mbele ya Hema la
Kukutania. Kisha wana wa Haruni watanyunyiza
damu ya huyo mnyama pande zote za mad-
habahu.
9 Katika hiyo sadaka ya amani ataleta dhabihu
iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto:
mafuta yake, mafuta yote ya mkia uliokatwa
karibu na uti wa mgongo, mafuta yote yanayofu-
nika sehemu za ndani au yale yanayounganika
nazo,
10 figo mbili pamoja na mafuta yanayozifunika
yaliyo karibu na kiuno, na kipande kirefu cha ini,
ambayo utayaondoa pamoja na figo.
11 Kuhani ataviteketeza juu ya madhabahu
viwe chakula, sadaka iliyotolewa kwa Mwenyezi
Mungu kwa moto.

12 “ ‘Ikiwa sadaka yake ni mbuzi, ataileta mbele
za Mwenyezi Mungu.
13 Ataweka mkono wake juu ya kichwa chake
na kumchinja mbele ya Hema la Kukutania.
Kisha wana wa Haruni watanyunyiza damu ya
huyo mnyama pande zote za madhabahu.
14 Katika ile sadaka anayotoa, atatoa hii sadaka
ya kuteketezwa kwa Mwenyezi Mungu: mafuta
yote yanayofunika sehemu za ndani na yale
yanayoungana nazo,
15 figo zote mbili pamoja na mafuta yaliyo juu

yake karibu na kiuno, na kipande kirefu cha ini,
ambayo atayaondoa pamoja na figo.
16 Kuhani ataviteketeza juu ya madhabahu
viwe chakula, sadaka iliyotolewa kwa moto,
harufu nzuri. Mafuta yote ya mnyama ni ya
Mwenyezi Mungu.
17 " 'Hili ni agizo la kudumu kwa vizazi vi-
javyo, popote mnapoishi: Msile mafuta yoyote ya
mnyama wala damu.' "

# 4

*Sadaka ya dhambi*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
2 "Waambie Waisraeli: 'Mtu yeyote afanyapo
dhambi bila kukusudia na akatenda lile
lililokatazwa katika amri yoyote ya Mwenyezi
Mungu:
3 " 'Ikiwa kuhani aliyepakwa mafuta amefanya
dhambi na kuwaletea watu hatia, lazima alete
kwa Mwenyezi Mungu fahali mchanga asiye na
dosari, kuwa sadaka ya dhambi kwa ajili ya
dhambi aliyotenda.
4 Atamkabidhi huyo fahali kwenye ingilio la
Hema la Kukutania mbele za Mwenyezi Mungu.
Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha huyo
fahali na kumchinja mbele za Mwenyezi Mungu.
5 Kisha kuhani huyo aliyepakwa mafuta at-
achukua sehemu ya damu ya huyo fahali na
kuileta katika Hema la Kukutania.
6 Atachovya kidole chake katika hiyo damu,
na kuinyunyiza sehemu yake mara saba mbele
za Mwenyezi Mungu, mbele ya pazia la mahali
patakatifu.

7 Kisha kuhani atatia sehemu ya hiyo damu juu
ya pembe za madhabahu ya kufukizia uvumba
wenye harufu nzuri iliyo mbele za Mwenyezi
Mungu katika Hema la Kukutania. Damu iliy-
obaki ya huyo fahali ataimwaga chini ya hayo
madhabahu ya kuteketezea sadaka kwenye in-
gilio la Hema la Kukutania.
8 Atayaondoa mafuta yote ya fahali huyo wa
sadaka ya dhambi: mafuta yale yanayofunika
sehemu za ndani au zile zinazounganika nazo,
9 figo zote mbili na mafuta yaliyo juu yake
karibu na kiuno, na kipande kirefu cha ini,
ambayo atayaondoa pamoja na figo zote,
10 kama vile mafuta yanavyoondolewa ku-
toka kwa ng'ombe aliyetolewa sadaka ya amani.
Kisha kuhani ataviteketeza juu ya madhabahu ya
sadaka ya kuteketezwa.
11 Lakini ngozi ya huyo fahali na nyama zake
zote, pamoja na kichwa na miguu yake, sehemu
za ndani na matumbo,
12 yaani sehemu nyingine zote zilizobaki za
huyo fahali, lazima azitoe nje ya kambi hadi
mahali palipo safi, ambapo majivu hutupwa;
naye atamchoma kwa moto wa kuni juu ya lundo
la majivu.

13 " 'Ikiwa jumuiya yote ya Israeli watatenda
dhambi pasipo kukusudia na kufanya lile
lililokatazwa katika amri yoyote ya Mwenyezi
Mungu, hata kama jumuiya hawafahamu jambo
hilo, wana hatia.
14 Wanapotambua dhambi waliyoitenda, laz-
ima kusanyiko walete fahali mchanga kuwa

sadaka ya dhambi, na kuikabidhi mbele ya Hema
la Kukutania.
15 Wazee wa jumuiya wataweka mikono
yao juu ya kichwa cha huyo fahali mbele za
Mwenyezi Mungu, naye huyo fahali atachinjwa
mbele za Mwenyezi Mungu.
16 Kisha kuhani aliyepakwa mafuta ataingiza
sehemu ya damu ya huyo fahali ndani ya Hema
la Kukutania.
17 Atachovya kidole chake kwenye damu na
kuinyunyiza mara saba mbele za Mwenyezi
Mungu mbele ya hilo pazia.
18 Atatia sehemu ya hiyo damu juu ya pembe
za madhabahu yaliyo mbele za Mwenyezi Mungu
katika Hema la Kukutania. Damu iliyobaki
ataimwaga chini ya madhabahu ya kuteketezea
sadaka, penye ingilio la Hema la Kukutania.
19 Atayaondoa mafuta yote ya yule fahali na
kuyateketeza juu ya madhabahu,
20 naye atamfanyia fahali huyu kama alivy-
omfanyia yule fahali mwingine wa sadaka ya
dhambi. Kwa njia hii kuhani atawafanyia watu
upatanisho, nao watasamehewa.
21 Kisha atamchukua yule fahali nje ya kambi
na kumteketeza kama alivyomteketeza yule wa
kwanza. Hii ni sadaka ya dhambi kwa ajili ya
jumuiya.

22 “ ‘Wakati kiongozi ametenda dhambi bila
kukusudia na kufanya yaliyokatazwa katika amri
yoyote ya Mwenyezi Mungu, Mungu wake, ana
hatia.
23 Atakapofahamishwa dhambi aliyotenda, ni
lazima alete beberu asiye na dosari kuwa sadaka

yake.
24 Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha
yule mbuzi na kumchinja mahali pale sadaka
za kuteketezwa huchinjiwa mbele za Mwenyezi
Mungu. Hii ni sadaka ya dhambi.
25 Kisha kuhani atachukua sehemu ya damu
ya sadaka ya dhambi kwa kidole chake na kuitia
kwenye pembe za madhabahu ya sadaka ya
kuteketeza, na kuimwaga damu iliyobaki chini
ya madhabahu.
26 Atayateketeza mafuta yote juu ya mad-
habahu, kama alivyoteketeza mafuta ya mnyama
wa sadaka ya amani. Kwa njia hii kuhani
atafanya upatanisho wa dhambi kwa ajili ya yule
mtu, naye atasamehewa.
27 " 'Kama mtu katika jumuiya ametenda
dhambi pasipo kukusudia, na kufanya lile
lililokatazwa katika amri yoyote ya Mwenyezi
Mungu, yeye ana hatia.
28 Atakapofahamishwa dhambi aliyoitenda, ni
lazima alete mbuzi jike asiye na dosari kuwa
sadaka yake kwa ajili ya dhambi aliyotenda.
29 Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha
sadaka ya dhambi na kumchinjia mahali pa
kuteketezea sadaka.
30 Kisha kuhani atachukua sehemu ya ile
damu kwa kidole chake na kuitia kwenye pembe
za madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa na
kuimwaga damu iliyobaki chini ya madhabahu.
31 Atayaondoa mafuta yote, kama vile mafuta
yaondolewavyo kwenye sadaka ya amani, naye
kuhani atayateketeza juu ya madhabahu kama
harufu nzuri ya kumpendeza Mwenyezi Mungu.

Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake, naye atasamehewa.

32 “ ‘Akileta mwana-kondoo kuwa sadaka yake ya dhambi, atamleta jike asiye na dosari.

33 Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha huyo mwana-kondoo na kumchinja kwa ajili ya sadaka ya dhambi mahali ambako sadaka ya kuteketezwa huchinjiwa.

34 Kisha kuhani atachukua sehemu ya damu ya sadaka ya dhambi kwa kidole chake na kuitia juu ya pembe za madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, na ile damu iliyobaki ataimwaga chini ya madhabahu.

35 Ataondoa mafuta yote, kama vile mafuta yaondolewavyo kutoka kwa mwana-kondoo wa sadaka ya amani, naye kuhani atayateketeza juu ya madhabahu juu ya zile sadaka zilizotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto. Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake kwa dhambi aliyoitenda, naye atasamehewa.

# 5

## *Sadaka zingine za kuondoa dhambi*

1 “ ‘Ikiwa mtu ametenda dhambi kwa sababu hakusema alipotakiwa kutoa ushahidi hadharani kuhusu jambo aliloona au kujua habari zake, yeye atastahili adhabu.

2 “ ‘Au mtu akitambua kuwa ana hatia, kama vile akigusa kitu chochote ambacho ni najisi, iwe ni mizoga ya wanyama pori walio najisi, au ya wanyama wafugwao walio najisi, au ya viumbe

vinavyotambaa ardhini, hata akiwa hana habari, amekuwa najisi na mwenye hatia.

3 " 'Au akigusa kitu kilicho kichafu kinachotokana na binadamu, kitu chochote kile kinachoweza kumfanya awe najisi, hata akiwa hana habari, atakapofahamu atakuwa na hatia.

4 " 'Au kama mtu ameapa kufanya kitu chochote bila kufikiri, kiwe chema au kibaya, kwa vyovyote mtu aweza kuapa bila kujali, hata akiwa hana habari, atakapofahamu atakuwa na hatia.

5 " 'Mtu yeyote atakapokuwa na hatia katika mojawapo ya haya, ni lazima akiri ni kwa njia gani ametenda dhambi,

6 na kama adhabu ya dhambi aliyoitenda, ni lazima alete kwa Mwenyezi Mungu kondoo jike au mbuzi jike kutoka kundi lake kuwa sadaka ya dhambi; naye kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake kwa dhambi yake.

7 " 'Lakini kama huyo mtu hataweza kumtoa mwana-kondoo, ataleta hua wawili au makinda wawili wa njiwa kwa Mwenyezi Mungu ikiwa ni adhabu kwa ajili ya dhambi yake: mmoja wa hao ndege kwa ajili ya sadaka ya dhambi, na wa pili kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa.

8 Atawaleta kwa kuhani, ambaye atamtoa kwanza ndege mmoja kwa ajili ya sadaka ya dhambi. Atamvunja shingo na kuacha kichwa chake kikining'inia,

9 naye atanyunyiza sehemu ya hiyo damu ya sadaka ya dhambi kwenye pembe za madhabahu. Damu iliyobaki lazima ichuruzwe chini ya madhabahu. Hii ni sadaka ya dhambi.

10 Kisha kuhani atamtoa yule ndege wa pili
kama sadaka ya kuteketezwa kwa kufuata utarat-
ibu uliowekwa, na hivyo kufanya upatanisho
kwa ajili yake kwa dhambi aliyoitenda, naye
atasamehewa.
11 “ ‘Ikiwa basi hawezi kupata hua wawili au
makinda wawili wa njiwa, ataleta sehemu ya
kumi ya efa* ya unga laini kwa ajili ya sadaka ya
dhambi. Kamwe asiweke mafuta wala uvumba
juu yake, kwa sababu ni sadaka ya dhambi.
12 Atauleta unga kwa kuhani, ambaye at-
achukua konzi moja kama sehemu ya kum-
bukumbu na atauteketeza kwenye madhabahu
juu ya sadaka zilizotolewa kwa Mwenyezi Mungu
kwa moto. Hii ni sadaka ya dhambi.
13 Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho kwa
ajili yake kwa dhambi yoyote ya hizo alizotenda,
naye atasamehewa. Sadaka iliyobaki itakuwa ya
kuhani, kama ilivyokuwa ile sadaka ya nafaka.’ ”

## *Sadaka ya hatia*

14 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa:
15 “Mtu anapokiuka na kutenda dhambi
pasipo kukusudia kuhusu mojawapo ya mambo
matakatifu ya Mwenyezi Mungu, huyo mtu
ataleta kwa Mwenyezi Mungu kama adhabu
kondoo dume mmoja kutoka kundi lake, asiye
na dosari, na mwenye thamani halisi ya fedha
kulingana na shekeli ya mahali patakatifu. Hii ni
sadaka ya hatia.

---

* **5:11** Sehemu ya kumi ya efa ni sawa na kilo moja.

16 Ni lazima alipe kwa yale aliyoshindwa ku-
fanya kuhusu vitu vitakatifu, kwa kuongeza se-
hemu ya tano ya thamani ile na kuitoa yote
kwa kuhani, ambaye atamfanyia upatanisho kwa
huyo kondoo dume kama sadaka ya dhambi,
naye atasamehewa.
17 “Kama mtu akifanya dhambi, na kutenda
yaliyokatazwa katika mojawapo ya amri za
Mwenyezi Mungu, hata ikiwa hajui, yeye ana
hatia na anastahili adhabu.
18 Atamletea kuhani kama sadaka ya hatia
kondoo dume kutoka kundi lake, kondoo asiye na
dosari na mwenye thamani halisi. Kwa njia hii,
kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake kwa
kosa alilotenda bila kukusudia, naye atasame-
hewa.
19 Hii ni sadaka ya hatia; amekuwa na hatia
kwa kufanya kosa dhidi ya Mwenyezi Mungu.”

# 6

*Kurudisha kilichochukuliwa*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa:
2 “Mtu yeyote akitenda dhambi, naye si
mwaminifu kwa Mwenyezi Mungu kwa
kumdanganya jirani yake kuhusu kitu fulani
alichokabidhiwa, au kimeachwa chini ya
utunzaji wake, au kimeibwa, au kama
akimdanganya,
3 au akiokota mali iliyopotea na akadanganya
kuihusu, au kuapa kwa uongo, au kama aki-
tenda dhambi yoyote ambayo watu wanaweza
kuitenda;

4 wakati akitenda dhambi hizo na kuwa mwenye hatia, ni lazima arudishe kile alichokuwa amekiiba au amekichukua kwa dhuluma, au alichokuwa amekabidhiwa, au mali iliyokuwa imepotea akaipata,
5 au chochote alichokuwa amekiapia kwa uongo. Lazima akirudishe kikamilifu, na aongeze sehemu ya tano ya thamani yake, vyote ampe mwenye mali siku ile anapeleka sadaka yake ya hatia.
6 Kisha kama adhabu lazima amletee kuhani, yaani kwa Mwenyezi Mungu, kuwa sadaka yake ya hatia, kondoo dume kutoka kundi lake asiye na dosari, mwenye thamani kamili.
7 Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake mbele za Mwenyezi Mungu, naye atasamehewa kwa kosa lolote katika mambo aliyoyatenda lililomfanya kuwa na hatia.”

### *Sadaka ya kuteketezwa*

8 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa:
9 “Mpe Haruni na wanawe agizo hili: ‘Haya ndio masharti kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa: Sadaka ya kuteketezwa itabaki kwenye moto juu ya madhabahu usiku kucha, hadi asubuhi, nao moto lazima uwe unaendelea kuwaka juu ya madhabahu.
10 Kisha kuhani atavaa mavazi yake ya kitani, pamoja na nguo za ndani za kitani mwilini wake, na aondoe majivu ya sadaka ya kuteketezwa ambayo moto umeteketeza juu ya madhabahu, na kuyaweka kando ya madhabahu.

11 Kisha atayavua mavazi haya na kuvaa
mengine, naye achukue yale majivu nje ya kambi
na kuyapeleka mahali palipo safi.
12 Moto ulio juu ya madhabahu lazima uwe un-
aendelea kuwaka; kamwe usizimike. Kila asub-
uhi kuhani ataongeza kuni na kupanga sadaka ya
kuteketezwa juu ya moto, na kuteketeza mafuta
ya wanyama wa sadaka za amani juu yake.
13 Moto lazima uendelee kuwaka juu ya mad-
habahu mfululizo, kamwe usizimike.

### *Sadaka ya nafaka*

14 " 'Haya ndio masharti ya sadaka ya nafaka:
Wana wa Haruni wataileta mbele za Mwenyezi
Mungu, mbele za madhabahu.
15 Kuhani atachukua konzi moja ya unga laini
na mafuta, pamoja na uvumba wote ulio juu ya
sadaka ya nafaka, na kuteketeza sehemu hiyo ya
kumbukumbu juu ya madhabahu kama harufu
nzuri ya kumpendeza Mwenyezi Mungu.
16 Haruni na wanawe watakula sehemu iliy-
obaki, lakini italiwa bila kutiwa chachu mahali
patakatifu, nao wataila katika ua wa Hema la
Kukutania.
17 Kamwe haitaokwa na chachu; nimewapa
kama fungu lao la sadaka iliyotolewa kwangu
kwa moto. Ni takatifu sana, kama vile ilivyo
sadaka ya dhambi na ya hatia.
18 Kila mwanaume mzao wa Haruni aweza
kuila. Ni fungu lake milele la sadaka zilizo-
tolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto kwa
vizazi vijavyo. Chochote kinachozigusa kitakuwa
kitakatifu.' "
19 Tena Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,

20 “Hii ni sadaka ambayo Haruni na wanawe
wanapaswa kuleta kwa Mwenyezi Mungu siku
atakapopakwa mafuta: sehemu ya kumi ya efa*
ya unga laini kama sadaka ya kawaida ya nafaka.
Nusu yake ataitoa asubuhi na nusu nyingine
jioni.
21 Iandae kwa mafuta kwenye kikaango; ilete
ikiwa imechanganywa vizuri, na utoe hiyo
sadaka ya nafaka ikiwa imevunjwa vipande
vipande kuwa harufu nzuri ya kumpendeza
Mwenyezi Mungu.
22 Mwanawe atakayeingia mahali pake kama
kuhani aliyepakwa mafuta ndiye atakayeiandaa.
Ni fungu la milele la Mwenyezi Mungu, nalo
litateketezwa kabisa.
23 Kila sadaka ya nafaka ya kuhani
itateketezwa kabisa; kamwe haitaliwa.”

*Sadaka ya dhambi*

24 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
25 “Mwambie Haruni na wanawe: ‘Haya ndio
masharti kwa ajili ya sadaka ya dhambi: Sadaka
ya dhambi itachinjiwa mbele za Mwenyezi
Mungu mahali sadaka ya kuteketezwa huchin-
jiwa; ni takatifu sana.
26 Kuhani anayeitoa ndiye atakayeikula;
itakuliwa katika mahali patakatifu, katika ua
wa Hema la Kukutania.
27 Chochote kitakachogusa nyama yoyote ya
hiyo sadaka kitakuwa kitakatifu; na kama damu
ya hiyo sadaka itadondokea juu ya vazi, lazima
ulifulie mahali patakatifu.

* **6:20** Sehemu ya kumi ya efa ni sawa na kilo moja.

28 Chungu cha udongo kitakachopikiwa nyama
lazima kivunjwe, lakini kama imepikiwa kwenye
chombo cha shaba, chombo hicho kitasuguliwa
na kusuuzwa kwa maji.
29 Kila mwanaume katika jamaa ya kuhani
aweza kula nyama hiyo; ni takatifu sana.
30 Lakini kila sadaka ya dhambi ambayo damu
yake imeletwa ndani ya Hema la Kukutania
kufanya upatanisho katika Mahali Patakatifu
kamwe haitaliwa; lazima iteketezwe.

# 7

*Sadaka ya hatia*

1 " 'Haya ndio masharti kwa ajili ya sadaka ya
hatia, ambayo ni takatifu sana:
2 Sadaka ya hatia itachinjiwa mahali pale
sadaka ya kuteketezwa huchinjiwa, nayo damu
yake itanyunyizwa pande zote za madhabahu.
3 Mafuta yake yote yatatolewa sadaka: mafuta
ya mkia, na mafuta yale yanayofunika sehemu za
ndani,
4 figo zote mbili pamoja na mafuta yanayozifu-
nika karibu na kiuno, na kipande kirefu cha ini,
ambayo yataondolewa pamoja na hizo figo.
5 Kuhani atayateketeza juu ya madhabahu
kuwa sadaka iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu
kwa moto. Hii ni sadaka ya hatia.
6 Mwanaume yeyote katika jamaa ya kuhani
aweza kuila, lakini lazima iliwe mahali patakat-
ifu; ni takatifu sana.
7 " 'Sheria hii ya sadaka ya hatia ni sawasawa
na ile ya sadaka ya dhambi: Nyama ya yule

mnyama aliyetolewa sadaka ni ya yule kuhani anayesimamia ibada ya upatanisho.
8 Kuhani anayetoa sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya mtu yeyote anaweza kuichukua ngozi ya mnyama yule aliyetolewa iwe yake.
9 Kila sadaka ya nafaka iliyookwa jikoni au kupikwa katika sufuria au katika kikaango itakuwa ya kuhani anayeitoa.
10 Nayo kila sadaka ya nafaka, iwe imechanganywa na mafuta au iko kavu, itakuwa ya wana wa Haruni, nayo itagawanywa sawa kati yao.

### *Sadaka ya amani*

11 “ ‘Haya ndio masharti kwa ajili ya sadaka ya amani ambayo mtu aweza kuileta kwa Mwenyezi Mungu:

12 “ ‘Ikiwa mtu atatoa sadaka ya amani kwa ajili ya kuonesha shukrani, pamoja na sadaka hii ya shukrani, atatoa maandazi yasiyotiwa chachu yaliyochanganywa na mafuta, mikate myembamba isiyotiwa chachu na iliyopakwa mafuta, na maandazi ya unga laini uliokandwa vizuri na kuchanganywa na mafuta.
13 Pamoja na sadaka yake ya amani ya shukrani, ataleta sadaka ya maandazi yaliyotengenezwa kwa chachu.
14 Ataleta moja ya kila aina ya andazi kuwa sadaka, matoleo kwa Mwenyezi Mungu; hii ni ya kuhani anayenyunyiza damu ya sadaka ya amani.

15 Nyama ya sadaka ya amani kwa ajili ya shukrani lazima iliwe siku hiyo hiyo inapotolewa; hutabakiza kitu chochote hadi asubuhi.
16 " 'Lakini ikiwa sadaka yake ni kwa ajili ya nadhiri au ni sadaka ya hiari, sadaka hiyo italiwa siku hiyo inapotolewa, lakini chochote kinachobakia kinaweza kuliwa kesho yake.
17 Nyama yoyote ya sadaka inayobaki hadi siku ya tatu lazima iteketezwe kwa moto.
18 Kama nyama yoyote ya sadaka ya amani italiwa siku ya tatu, Mwenyezi Mungu hataikubali. Haitahesabiwa kwake huyo aliyeitoa, kwa kuwa ni najisi. Mtu atakayekula sehemu yake yoyote atahesabiwa hatia.
19 " 'Nyama inayogusa chochote kilicho najisi kamwe haitaliwa; lazima iteketezwe kwa moto. Kuhusu nyama nyingine, mtu yeyote aliyetakaswa anaweza kuila.
20 Lakini kama mtu yeyote najisi akila nyama yoyote ya sadaka ya amani iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu, huyo mtu lazima akatiliwe mbali na watu wake.
21 Kama mtu yeyote akigusa kitu kilicho najisi, iwe ni uchafu wa mwanadamu, au mnyama najisi, au kitu chochote kilicho najisi, kitu cha kuchukiza, kisha akala nyama yoyote ya sadaka ya amani iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu, mtu huyo ni lazima akatiliwe mbali na watu wake.' "

### *Kula mafuta na kunywa damu kwakatazwa*

22 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
23 "Waambie Waisraeli: 'Msile mafuta yoyote ya ng'ombe, kondoo wala mbuzi.

24 Mafuta ya mnyama aliyekutwa amekufa au
amereruliwa na wanyama pori yanaweza kutu-
mika kwa kazi nyingine yoyote, lakini kamwe
msiyale.
25 Mtu yeyote alaye mafuta ya mnyama ambaye
ametolewa sadaka kwa Mwenyezi Mungu kwa
moto ni lazima akatiliwe mbali na watu wake.
26 Popote mtakapoishi, kamwe msile damu ya
ndege yeyote wala ya mnyama.
27 Mtu yeyote atakayekula damu lazima
akatiliwe mbali na watu wake.' "

*Fungu la makuhani*

28 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
29 "Waambie Waisraeli: 'Mtu yeyote aletaye
sadaka ya amani kwa Mwenyezi Mungu ataleta
sehemu ya sadaka hiyo kama dhabihu yake kwa
Mwenyezi Mungu.
30 Ataleta sadaka kwa mikono yake mwenyewe
iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto;
ataleta mafuta ya huyo mnyama pamoja na
kidari, naye atainua hicho kidari mbele za
Mwenyezi Mungu kuwa sadaka ya kuinuliwa.
31 Kuhani atayateketeza hayo mafuta juu ya
madhabahu, lakini kidari kitakuwa cha Haruni
na wanawe.
32 Paja la kulia la sadaka zako za amani utampa
kuhani kama matoleo.
33 Mwana wa Haruni atoaye damu na
mafuta ya mnyama wa sadaka ya amani ndiye
atakayepewa paja hilo la kulia kuwa fungu lake.
34 Kutoka kwa sadaka za amani za Waisraeli,
mimi Mungu nimepokea kidari kile kilichoin-
uliwa, pamoja na lile paja lililotolewa, nami

nimevitoa kwa kuhani Haruni na wanawe kuwa fungu lao la milele kutoka kwa Waisraeli.' "

35 Hii ndiyo sehemu ya sadaka zilizotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto, ambazo zilitengwa kwa ajili ya Haruni na wanawe siku ile walipowekwa wakfu ili kumtumikia Mwenyezi Mungu katika kazi ya ukuhani.

36 Siku ile walipopakwa mafuta, Mwenyezi Mungu aliagiza kwamba Waisraeli wawape hili kama fungu lao la milele kwa vizazi vijavyo.

37 Basi haya ndio masharti kuhusu sadaka ya kuteketezwa, sadaka ya nafaka, sadaka ya dhambi, sadaka ya hatia, sadaka ya kuwekwa wakfu, na sadaka ya amani,

38 ambayo Mwenyezi Mungu alimpa Musa juu ya Mlima Sinai siku ile alipowaagiza Waisraeli walete sadaka zao kwa Mwenyezi Mungu, katika Jangwa la Sinai.

# 8

### *Kuwekwa wakfu kwa Haruni na wanawe (Kutoka 29:1-37)*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,

2 "Waletee Haruni na wanawe mavazi yao, mafuta ya upako, fahali kwa ajili ya sadaka ya dhambi, kondoo dume wawili na kikapu chenye mikate iliyotengenezwa bila chachu.

3 Kisha kusanya watu wote kwenye ingilio la Hema la Kukutania."

4 Musa akafanya kama Mwenyezi Mungu alivyomwagiza, na watu wakakusanyika kwenye ingilio la Hema la Kukutania.

5 Musa akawaambia kusanyiko, “Hili ndilo Mwenyezi Mungu ameagiza lifanyike.”
6 Kisha Musa akamleta Haruni na wanawe mbele, akawaosha kwa maji.
7 Akamvika Haruni koti, akamfunga mshipi, akamvika joho, na kumvalisha kizibau. Pia akamfunga hicho kizibau kiunoni mwake kwa mshipi uliofumwa kwa ustadi.
8 Akaweka kifuko cha kifuani juu yake, na kuweka Urimu na Thumimu* kwenye hicho kifuko.
9 Kisha akamvika Haruni kilemba kichwani pake, akaweka lile bamba la dhahabu, lile taji takatifu, upande wa mbele wa kilemba, kama Mwenyezi Mungu alivyomwagiza Musa.
10 Kisha Musa akachukua mafuta ya upako, na kuipaka maskani ya Mungu na kila kitu kilichokuwamo; hivyo akaviweka wakfu.
11 Akanyunyiza sehemu ya mafuta juu ya madhabahu mara saba, akaipaka madhabahu mafuta na vyombo vyake vyote, pamoja na sinia na kinara chake, ili kuviweka wakfu.
12 Akamimina sehemu ya hayo mafuta ya upako kichwani mwa Haruni, akampaka mafuta ili kumweka wakfu.
13 Kisha akawaleta wana wa Haruni mbele, akawavika makoti, akawafunga mishipi na kuwavika vilemba, kama Mwenyezi Mungu alivyomwagiza Musa.

* **8:8** Urimu na Thumimu maana yake ni Nuru na Kweli; vifaa hivi viliwekwa kwenye kifuko cha juu cha kisibau cha kuhani mkuu ili kujua mapenzi ya Mungu kwenye mambo ya kutatanisha.

14 Kisha akamtoa fahali kwa ajili ya sadaka
ya dhambi, nao Haruni na wanawe wakaweka
mikono yao juu ya kichwa chake.
15 Musa akamchinja yule fahali na akachukua
sehemu ya hiyo damu, kisha kwa kidole chake
akaitia kwenye pembe zote za madhabahu ili
kutakasa madhabahu. Akaimwaga damu iliy-
obaki chini ya madhabahu. Kwa hiyo akayaweka
wakfu ili kufanya upatanisho kwa ajili ya mad-
habahu.
16 Pia Musa akachukua mafuta yote yanayofu-
nika sehemu za ndani, na kipande kirefu cha
ini, na figo zote mbili pamoja na mafuta yake,
akayateketeza juu ya madhabahu.
17 Lakini fahali, ikiwa pamoja na ngozi yake
na nyama yake na sehemu zake za ndani na
matumbo, akaiteketeza nje ya kambi, kama
Mwenyezi Mungu alivyomwagiza Musa.

18 Kisha Musa akamleta kondoo dume kwa
ajili ya sadaka ya kuteketezwa, naye Haruni na
wanawe wakaweka mikono yao juu ya kichwa
chake.
19 Ndipo Musa akamchinja yule kondoo dume
na kunyunyiza damu yake pande zote za mad-
habahu.
20 Musa akamkata yule kondoo dume vipande
vipande na kukiteketeza kichwa, vile vipande na
yale mafuta.
21 Kisha akamsafisha sehemu za ndani na
miguu kwa maji, na kumteketeza yule kondoo
dume mzima juu ya madhabahu kuwa sadaka ya
kuteketezwa, harufu nzuri ya kupendeza, sadaka
iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto,

kama Mwenyezi Mungu alivyomwagiza Musa.

22 Kisha Musa akamleta yule kondoo dume wa
pili, ndiye kondoo dume kwa ajili ya kuwaweka
wakfu, naye Haruni na wanawe wakaweka
mikono yao juu ya kichwa chake.
23 Musa akamchinja yule kondoo dume,
akaichukua sehemu ya damu yake na kuipaka
juu ya ncha ya sikio la kuume la Haruni, na juu
ya kidole gumba cha mkono wake wa kuume
na juu ya kidole kikubwa cha mguu wake wa
kuume.
24 Pia Musa akawaleta hao wana wa Haruni
mbele, akaipaka sehemu ya hiyo damu kwenye
ncha za masikio yao ya kuume, juu ya vidole
gumba vya mikono yao ya kuume, na juu ya
vidole vikubwa vya miguu yao ya kuume. Kisha
akanyunyiza damu pande zote za madhabahu.
25 Akachukua mafuta ya mnyama, mafuta ya
mkia, mafuta yote yanayofunika sehemu za
ndani, kipande kirefu cha ini, figo zote mbili
pamoja na mafuta yake, na paja la kulia.
26 Kisha kutoka kwa kikapu cha mikate iliy-
otengenezwa bila chachu, kilichokuwa mbele za
Mwenyezi Mungu, akachukua andazi moja, na
jingine lililotengenezwa kwa mafuta, na mkate
mwembamba; akaviweka hivi vyote juu ya ma-
fungu ya mafuta ya mnyama, na juu ya lile paja
la kulia.
27 Akaviweka hivi vyote mikononi mwa Haruni
na wanawe, na kuviinua mbele za Mwenyezi
Mungu kuwa sadaka ya kuinuliwa.
28 Kisha Musa akavichukua kutoka mikononi
mwao na kuviteketeza juu ya madhabahu

ya sadaka ya kuteketezwa kuwa sadaka ya kuwekwa wakfu, harufu nzuri ya kupendeza, sadaka iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto.
29 Kisha akachukua kidari, kilicho fungu la Musa la kondoo dume kwa ajili ya kuwekwa wakfu, na kukiinua mbele za Mwenyezi Mungu kuwa sadaka ya kuinuliwa, kama Mwenyezi Mungu alivyomwagiza Musa.

30 Kisha Musa akachukua sehemu ya mafuta ya upako, na sehemu ya damu kutoka madhabahu, na kuvinyunyiza juu ya Haruni na mavazi yake, na juu ya wanawe na mavazi yao. Kwa hiyo akamweka Haruni na mavazi yake wakfu, pamoja na wanawe na mavazi yao.

31 Kisha Musa akamwambia Haruni na wanawe, “Pikeni hiyo nyama kwenye ingilio la Hema la Kukutania, na muile hapo pamoja na mkate kutoka kikapu cha sadaka ya kuweka wakfu, kama nilivyoagiza: ‘Haruni na wanawe wataila.’
32 Kisha mteketeze nyama na mikate iliyobaki.
33 Msitoke kwenye ingilio la Hema la Kukutania kwa muda wa siku saba, hadi siku zenu za kuwekwa wakfu ziwe zimetimia, kwa kuwa muda wenu wa kuwekwa wakfu utakuwa siku saba.
34 Lile lililofanyika leo liliagizwa na Mwenyezi Mungu ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu.
35 Lazima mkae kwenye ingilio la Hema la Kukutania usiku na mchana kwa siku saba, na kufanya lile Mwenyezi Mungu analolitaka, ili msife; kwa kuwa hilo ndilo nililoamriwa.”

36 Kwa hiyo Haruni na wanawe wakafanya kila
kitu Mwenyezi Mungu alichoamuru kupitia kwa
Musa.

# 9

### *Makuhani waanza huduma yao*

1 Katika siku ya nane, Musa akawaita Haruni
na wanawe, na wazee wa Israeli.
2 Akamwambia Haruni, "Chukua ndama dume
kwa ajili ya sadaka yako ya dhambi, na kondoo
dume kwa sadaka yako ya kuteketezwa, wote
wawili wasiwe na dosari, nao uwalete mbele za
Mwenyezi Mungu.
3 Kisha waambie Waisraeli: 'Chukueni beberu
kwa ajili ya sadaka ya dhambi, na ndama na
mwana-kondoo, wote wawili wawe wa umri wa
mwaka mmoja, na wasio na dosari, kwa ajili ya
sadaka ya kuteketezwa,
4 na pia maksai na kondoo dume kwa ajili ya
sadaka ya amani, ili kutoa dhabihu mbele za
Mwenyezi Mungu, pamoja na sadaka ya nafaka
iliyochanganywa na mafuta. Kwa kuwa leo
Mwenyezi Mungu atawatokea.' "
5 Wakavileta vile vitu Musa alivyowaagiza
mbele ya Hema la Kukutania, na kusanyiko lote
wakakaribia na kusimama mbele za Mwenyezi
Mungu.
6 Ndipo Musa akasema, "Hili ndilo Mwenyezi
Mungu alilowaagiza mlifanye, ili utukufu wa
Mwenyezi Mungu upate kuonekana kwenu."
7 Musa akamwambia Haruni, "Njoo mad-
habahuni utoe dhabihu ya sadaka ya dhambi na
sadaka ya kuteketezwa, kuwa upatanisho kwa

ajili yako mwenyewe na kwa ajili ya watu. Kisha utoe sadaka ya upatanisho kwa ajili ya watu, kama vile Mwenyezi Mungu alivyoagiza.”

8 Hivyo Haruni akaja madhabahuni na kum-
chinja yule ndama kuwa sadaka ya dhambi kwa
ajili yake mwenyewe.
9 Wanawe wakamletea damu, naye akachovya
kidole chake katika hiyo damu, akaitia kwenye
pembe za madhabahu, nayo damu iliyobaki
akaimwaga chini ya madhabahu.
10 Juu ya madhabahu akateketeza mafuta, figo
na kipande kirefu cha ini kutoka hiyo sadaka ya
dhambi, kama Mwenyezi Mungu alivyomwagiza
Musa.
11 Akateketeza nyama na ngozi nje ya kambi.

12 Kisha Haruni akachinja sadaka ya
kuteketezwa. Wanawe wakamletea damu, naye
akainyunyiza pande zote za madhabahu.
13 Wakamletea sadaka ya kuteketezwa
kipande kwa kipande, pamoja na kichwa, naye
akaviteketeza juu ya madhabahu.
14 Akasafisha sehemu za ndani na miguu,
akaviteketeza juu ya sadaka ya kuteketezwa juu
ya madhabahu.

15 Kisha Haruni akaleta sadaka ile iliyokuwa
kwa ajili ya watu. Akachukua yule mbuzi wa
sadaka ya dhambi kwa ajili ya watu, akamchinja
na kumtoa kwa ajili ya sadaka ya dhambi, kama
alivyofanya kwa ile ya kwanza.

16 Haruni akaleta sadaka ya kuteketezwa na
kuitoa kama ilivyoelekezwa.

17 Pia akaleta sadaka ya nafaka, akachukua
konzi moja na kuiteketeza juu ya madhabahu,
pamoja na sadaka ya kuteketezwa ya asubuhi.

18 Akachinja maksai na kondoo dume kuwa
sadaka ya amani kwa ajili ya watu. Wanawe
Haruni wakampa ile damu, naye akainyunyiza
pande zote za madhabahu.
19 Lakini sehemu zile za mafuta ya yule maksai
na ya yule kondoo dume, yaani mafuta ya mkia,
yaliyofunika tumbo, ya figo na kipande kirefu
cha ini,
20 hivi vyote wakaviweka juu ya vidari, kisha
Haruni akayateketeza hayo mafuta ya wanyama
juu ya madhabahu.
21 Haruni akaviinua vile vidari na paja la kulia
mbele za Mwenyezi Mungu ili viwe sadaka ya
kuinuliwa, kama Musa alivyoagiza.

22 Kisha Haruni akainua mikono yake
kuwaelekea watu na kuwabariki. Naye baada
ya kutoa dhabihu ya sadaka ya dhambi, sadaka
ya kuteketezwa, na sadaka ya amani, akashuka
chini.

23 Kisha Musa na Haruni wakaingia
kwenye Hema la Kukutania. Walipotoka nje,
wakawabariki watu. Nao utukufu wa Mwenyezi
Mungu ukawatokea watu wote.
24 Moto ukaja kutoka kwa uwepo wa Mwenyezi
Mungu, ukaiteketeza ile sadaka ya kuteketezwa,
pamoja na sehemu ya mafuta yaliyokuwa juu ya
madhabahu. Watu wote walipoona jambo hili,
wakashangilia kwa furaha na kusujudu.

# 10

## *Kifo cha Nadabu na Abihu*

1 Nadabu na Abihu, wana wa Haruni, wakachukua vyetezo vyao, wakaweka moto ndani yake na kuongeza uvumba; kisha wakamtolea Mwenyezi Mungu moto usio halali, kinyume na agizo la Mungu.
2 Hivyo moto ukaja kutoka kwa uwepo wa Mwenyezi Mungu na kuwateketeza, nao wakafa mbele za Mwenyezi Mungu.
3 Kisha Musa akamwambia Haruni, "Hili ndilo alilonena Mwenyezi Mungu, aliposema:
" 'Miongoni mwa wale watakaonikaribia
nitajionesha kuwa mtakatifu;
machoni pa watu wote
nitaheshimiwa.' "
Haruni akanyamaza.
4 Musa akawaita Mishaeli na Elisafani, wana wa Uzieli mjomba wake Haruni, akawaambia, "Njooni hapa. Ondoeni miili ya ndugu zenu mbele ya mahali patakatifu, mkaipeleke nje ya kambi."
5 Hivyo wakaja na kuwaondoa, wakiwa bado wamevalia makoti yao ya ibada, wakawapeleka nje ya kambi, kama Musa alivyoamuru.
6 Ndipo Musa akamwambia Haruni pamoja na wanawe, Eleazari na Ithamari, "Msifunue vichwa vyenu wala msirarue mavazi yenu, la sivyo mtakufa na Mwenyezi Mungu ataikasirikia jumuiya nzima. Lakini ndugu zenu, nyumba yote ya Israeli, wanaweza kuwaombolezea wale ambao Mwenyezi Mungu amewaangamiza kwa moto.

7 Msitoke nje ya ingilio la Hema la Kukuta-
nia, la sivyo mtakufa, kwa sababu mafuta ya
Mwenyezi Mungu ya upako yako juu yenu."
Hivyo wakafanya kama vile Musa alivyosema.
8 Kisha Mwenyezi Mungu akamwambia
Haruni,
9 "Wewe na wanao msinywe mvinyo wala kiny-
waji kingine kilichochachuka wakati mwingiapo
katika Hema la Kukutania, la sivyo mtakufa. Hili
litakuwa agizo la kudumu kwa vizazi vijavyo.
10 Ni lazima mtenganishe kati ya kilicho ki-
takatifu na kilicho cha kawaida, kati ya kilicho
najisi na kilicho safi,
11 na lazima mwafundishe Waisraeli amri
zote ambazo Mwenyezi Mungu aliwapa kupitia
Musa."
12 Musa akamwambia Haruni pamoja na
wanawe waliosalia, Eleazari na Ithamari,
"Chukueni sadaka ya nafaka iliyobaki kutoka
kwa sadaka zilizotolewa kwa Mwenyezi Mungu
kwa moto, muile hapo kando ya madhabahu
ikiwa imeandaliwa bila chachu, kwa sababu ni
takatifu sana.
13 Mtaila katika mahali patakatifu kwa sababu
ni fungu lenu na fungu la wana wenu la sadaka
zilizotolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa moto,
kwa maana hivyo ndivyo nilivyoamriwa.
14 Lakini wewe na wanao na binti zako
mwaweza kula kidari kile kilichoinuliwa na paja
lile lililotolewa. Mtavila katika mahali patakat-
ifu; mmepewa wewe na wanao kuwa fungu lenu
la sadaka za amani za Waisraeli.
15 Paja lile lililotolewa na kidari kile kilichoin-
uliwa lazima viletwe pamoja na sehemu za

mafuta ya wanyama wa sadaka za kuteketezwa kwa moto, ili kuinuliwa mbele za Mwenyezi Mungu kuwa sadaka ya kuinuliwa. Hili litakuwa fungu lako na wanao milele, kama Mwenyezi Mungu alivyoagiza."

16 Musa alipouliza kuhusu mbuzi aliyetolewa
sadaka ya dhambi na kugundua kwamba ame-
teketezwa, aliwakasirikia Eleazari na Ithamari,
wana wa Haruni waliobaki. Akawauliza,
17 "Kwa nini hamkula sadaka ya dhambi katika
eneo la mahali patakatifu? Ni takatifu sana.
Mlipewa ninyi ili kuondoa hatia ya jumuiya
kwa ajili ya kuwafanyia upatanisho mbele za
Mwenyezi Mungu.
18 Kwa kuwa damu yake haikuletwa ndani ya
Mahali Patakatifu, mngemla mbuzi huyo katika
sehemu ya mahali patakatifu kama nilivyoagiza."
19 Haruni akamjibu Musa, "Leo wanangu
wametoa sadaka zao za dhambi na sadaka zao
za kuteketezwa mbele za Mwenyezi Mungu,
lakini mambo kama haya yamenitokea mimi.
Je, Mwenyezi Mungu angependezwa kama
ningekuwa nimekula sadaka ya dhambi leo?"
20 Musa aliposikia haya, akaridhika.

# 11

*Vyakula najisi na visivyo najisi*
*(Kumbukumbu 14:3-21)*

1 Mwenyezi Mungu akawaambia Musa na
Haruni,
2 "Waambieni Waisraeli: 'Kati ya wanyama
wote wanaoishi juu ya nchi, hawa ndio
mtakaowala:

3 Mwaweza kula mnyama yeyote mwenye kwato zilizogawanyika sehemu mbili na ambaye hucheua.
4 “ ‘Kuna wanyama wengine ambao hucheua tu au wenye kwato zilizogawanyika tu, lakini hao kamwe msiwale. Ngamia ingawa hucheua, hana kwato zilizogawanyika; huyo ni najisi kwenu.
5 Pelele ingawa hucheua hana kwato zilizogawanyika; huyo ni najisi kwenu.
6 Sungura ingawa hucheua hana kwato zilizogawanyika; huyo ni najisi kwenu.
7 Naye nguruwe ingawa anazo kwato zilizogawanyika sehemu mbili, hacheui; huyo ni najisi kwenu.
8 Kamwe msile nyama yao wala kugusa mizoga yao; wao ni najisi kwenu.

9 “ ‘Kuhusu viumbe wote wanaoishi ndani ya maji ya bahari na vijito, mtakula wale wote wenye mapezi na magamba.
10 Lakini viumbe wote ndani ya bahari au vijito wasio na mapezi na magamba, wakiwa miongoni mwa makundi au viumbe wote ndani ya maji, hao ni machukizo kwenu.
11 Nao watakuwa machukizo kwenu. Msile nyama yao, nayo mizoga yao itakuwa machukizo.
12 Chochote kinachoishi ndani ya maji ambacho hakina mapezi na magamba kitakuwa chukizo kwenu.
13 “ ‘Wafuatao ndio ndege watakaokuwa machukizo kwenu, hivyo msiwale kwa sababu ni chukizo: tai, furukombe, kipungu,
14 mwewe mwekundu, aina zote za mwewe mweusi,

15 aina zote za kunguru,
16 mbuni, kiruka-njia, dudumizi, kipanga, shakwe, aina zote za kipanga,
17 bundi, mnandi, bundi mkubwa,
18 mumbi, mwari, nderi,
19 korongo, koikoi wa aina yoyote, hudihudi na popo.
20 " 'Wadudu wote warukao ambao hutembea kwa miguu minne watakuwa chukizo kwenu.
21 Lakini kuna viumbe wenye mabawa ambao hutembea kwa miguu minne mtakaowala: wale wenye vifundo katika miguu yao ya kurukaruka juu ya ardhi.
22 Miongoni mwa hawa, mtakula nzige wa aina zote, senene, parare au panzi.
23 Lakini viumbe wengine wote wenye mabawa na wenye miguu minne ni machukizo kwenu.

## *Wanyama walio najisi*

24 " 'Mtajinajisi kwa wanyama hawa. Yeyote agusaye mizoga yao atakuwa najisi hadi jioni.
25 Yeyote atakayebeba mizoga ya viumbe hawa ni lazima afue nguo zake, naye atakuwa najisi hadi jioni.
26 " 'Kila mnyama mwenye ukwato ulioachana lakini haukugawanyika kabisa, au yule asiyecheua, huyo ni najisi kwenu; yeyote agusaye mzoga wowote wa hao atakuwa najisi.
27 Miongoni mwa wanyama wote wanaotembea kwa miguu minne, wale wanaotembea kwa vitanga vyao ni najisi kwenu; yeyote agusaye mizoga yao atakuwa najisi hadi jioni.

28 Yeyote atakayebeba mizoga yao ni lazima
afue nguo zake, naye atakuwa najisi hadi jioni.
Wanyama hawa ni najisi kwenu.

29 “ ‘Kuhusu wanyama watambaao juu ya ardhi,
hawa ni najisi kwenu: kicheche, panya, aina
yoyote ya mijusi mikubwa,
30 guruguru, kenge, mijusi ya ukutani, goromoe
na kinyonga.
31 Miongoni mwa wanyama wote wanaotam-
baa juu ya ardhi, hawa ni najisi kwenu. Yeyote
agusaye mizoga yao atakuwa najisi hadi jioni.
32 Ikiwa mmoja wao atakufa na kuangukia juu
ya kitu fulani, chombo hicho, hata kikiwa cha
matumizi gani, kitakuwa najisi, kiwe kimeten-
genezwa kwa mti, nguo, ngozi au gunia. Kiweke
ndani ya maji; kitakuwa najisi hadi jioni, kisha
kitakuwa safi tena.
33 Ikiwa mmoja wa wanyama aliyekufa ataan-
gukia ndani ya chungu, kila kilichomo katika
chungu hicho kitakuwa najisi, nawe ni lazima
uvunje chungu hicho.
34 Chakula chochote ambacho chaweza kuliwa
lakini kikawa kimeingia maji kutoka chungu
hicho ni najisi, na kitu chochote cha majimaji am-
bacho chaweza kunyweka kutoka chungu hicho
ni najisi.
35 Chochote ambacho mzoga utaangukia ki-
takuwa najisi. Jiko au chungu cha kupikia ni
lazima kivunjwe. Ni najisi, nawe ni lazima
uvihesabu kuwa najisi.
36 Lakini chemchemi au kisima, mahali
yanapokusanyika maji, patakuwa safi; lakini
yeyote atakayegusa moja ya mizoga hii ni najisi.

37 Kama mzoga ukianguka juu ya mbegu zozote ambazo ni za kupanda, zinabaki safi.
38 Lakini kama mbegu imetiwa maji na mzoga ukaanguka juu yake, hiyo mbegu ni najisi kwenu.

39 " 'Kama mnyama ambaye mnaruhusiwa kumla akifa, yeyote atakayeugusa mzoga wake atakuwa najisi hadi jioni.
40 Yeyote atakayekula sehemu ya mzoga huo ni lazima afue nguo zake, naye atakuwa najisi hadi jioni. Yeyote atakayebeba mzoga huo ni lazima afue nguo zake, naye atakuwa najisi hadi jioni.

41 " 'Kila kiumbe kinachotambaa juu ya ardhi ni chukizo; kisiliwe.
42 Msile kiumbe chochote kinachotambaa juu ya ardhi, kiwe kinachotambaa kwa tumbo lake, au kinachotambaa kwa miguu minne au kwa miguu mingi; ni chukizo.
43 Msijitie unajisi kwa kiumbe chochote kati ya hivi. Msijitie unajisi kwa viumbe hivyo au kutiwa unajisi navyo.
44 Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu; jitakaseni mwe watakatifu, kwa sababu mimi ni mtakatifu. Msijitie unajisi kwa kiumbe chochote kile kiendacho juu ya ardhi.
45 Mimi ndimi Mwenyezi Mungu niliyewapandisha mtoke Misri ili niwe Mungu wenu. Kwa hiyo kuweni watakatifu kwa sababu Mimi ni mtakatifu.

46 " 'Haya ndio masharti kuhusu wanyama, ndege, kila kiumbe hai kiendacho ndani ya maji, na kila kiumbe kiendacho juu ya ardhi.

47 Ni lazima mpambanue kati ya kilicho najisi
na kilicho safi, kati ya viumbe hai vinavyoweza
kuliwa na vile visivyoweza kuliwa.' "

# 12

## *Utakaso baada ya kuzaa mtoto*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
2 "Waambie Waisraeli: 'Mwanamke ambaye at-
apata mimba na kuzaa mtoto wa kiume atakuwa
najisi kwa siku saba, kama anavyokuwa najisi
wakati wa siku zake za hedhi.
3 Naye huyo mtoto atatahiriwa siku ya nane.
4 Kisha ni lazima huyo mwanamke asubiri
kwa siku thelathini na tatu, ndipo atakaswe
kutoka damu kwake. Hataruhusiwa kugusa kitu
chochote kilicho kitakatifu au kuingia mahali
patakatifu, hadi siku za kutakaswa kwake zime-
timia.
5 Kama alimzaa mtoto wa kike, mwanamke
huyo atakuwa najisi kwa majuma mawili, kama
wakati wake wa hedhi. Kisha atasubiri kwa siku
sitini na sita, ndipo atatakaswa kutoka damu
kwake.
6 " 'Siku zake za utakaso kwa ajili ya mwana au
binti zitakapotimia, mwanamke huyo atamletea
kuhani kwenye ingilio la Hema la Kukutania
mwana-kondoo mwenye umri wa mwaka mmoja
kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, na kinda la
njiwa au hua kwa ajili ya sadaka ya dhambi.
7 Atavitoa mbele za Mwenyezi Mungu ili
kufanya upatanisho kwa ajili yake, na kisha
atatakasika kutokana na kutokwa na damu.

“ ‘Haya ndio masharti kwa ajili ya mwanamke atakayezaa mtoto wa kiume au wa kike.
8 Kama huyo mwanamke hana uwezo wa kumpata mwana-kondoo, ataleta hua wawili au makinda wawili wa njiwa, mmoja kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa na mwingine kwa ajili ya sadaka ya dhambi. Kwa njia hii, kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake, naye atakuwa safi.’ ”

# 13

*Masharti kuhusu magonjwa ya ngozi yaambukizayo*

1 Mwenyezi Mungu akawaambia Musa na Haruni,
2 “Iwapo mtu yeyote atakuwa na uvimbe, au upele, au alama nyeupe juu ya ngozi yake, ambayo yaweza kuwa ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza*, ni lazima aletwe kwa kuhani Haruni, au kwa mmoja wa wanawe, hao makuhani.
3 Kuhani atachunguza hicho kidonda kilichopo juu ya ngozi yake, na kama nywele za mahali palipo na kidonda zimebadilika kuwa nyeupe, na ikiwa kidonda kimeingia ndani ya ngozi, basi ni ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza, yaani ukoma. Kuhani atakapomchunguza, atamtangaza mtu huyo kuwa najisi.
4 Kama alama juu ya ngozi yake ni nyeupe, lakini haionekani kuingia ndani ya ngozi, na nywele kwenye alama hiyo hazijageuka kuwa

* **13:2** yaani *ukoma*; ni neno lililotumika kueleza magonjwa mbalimbali ya ngozi, ambayo si lazima yawe ni ukoma halisi (pia 13:47)

nyeupe, kuhani atamtenga mtu aliyeambukizwa kwa siku saba.
5 Siku ya saba, kuhani atamchunguza, na kama hakuona badiliko kwenye kile kidonda na hakijaenea juu ya ngozi, atamtenga kwa siku nyingine saba.
6 Siku ya saba kuhani atamchunguza tena, na kama kidonda kimepungua na hakijaenea juu ya ngozi, kuhani atamtangaza mtu huyo kuwa ni safi; ni upele tu. Ni lazima mtu huyo afue mavazi yake, naye atakuwa safi.
7 Lakini ikiwa ule upele utaenea katika ngozi yake baada ya yeye kujionesha kwa kuhani na kutangazwa kuwa safi, ni lazima aende tena kwa kuhani.
8 Kuhani atamchunguza, na kama upele umeenea kwenye ngozi, atamtangaza kuwa najisi, kwani ni ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza.

9 “Wakati mtu yeyote ana ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza, ni lazima aletwe kwa kuhani.
10 Kuhani atamchunguza na kama kuna uvimbe mweupe katika ngozi ambao umefanya nywele kuwa nyeupe, na kama kuna nyama mbichi ndani ya uvimbe,
11 ni ugonjwa sugu wa ngozi, na kuhani atamtangaza kuwa najisi. Hatamtenga tena kwa sababu ni najisi tayari.

12 “Ikiwa ugonjwa utakuwa umeenea kwenye ngozi yake yote kwa kadiri kuhani atakavyoweza kuona, kwamba umeenea kwenye ngozi yote ya huyo mgonjwa kutoka kichwani hadi wayo,
13 kuhani atamchunguza, na kama ugonjwa umeenea mwili mzima, atamtangaza huyo mtu

kuwa safi. Kwa kuwa mwili wote umekuwa
mweupe, yeye ni safi.
14 Lakini itokeapo nyama mbichi kwenye ngozi
yake, atakuwa najisi.
15 Kuhani atakapoiona hiyo nyama mbichi,
atamtangaza mtu huyo kuwa najisi. Hiyo nyama
mbichi ni najisi, ana ugonjwa wa kuambukiza.
16 Hiyo nyama mbichi ikigeuka na kuwa nye-
upe, ni lazima amwendee kuhani.
17 Kuhani atamchunguza, na kama vidonda
vimekuwa vyeupe, kuhani atamtangaza
mgonjwa huyo kuwa safi; kisha atakuwa safi.

18 "Wakati mtu ana jipu juu ya ngozi yake nalo
likapona,
19 napo mahali palipokuwa na jipu pakatokea
uvimbe mweupe, au alama yenye wekundu na
weupe, ni lazima akajioneshe kwa kuhani.
20 Kuhani atapachunguza, na kama uvimbe
umeingia ndani ya ngozi, na nywele zimegeuka
kuwa nyeupe, kuhani atamtangaza mtu huyo
kuwa najisi. Ni ugonjwa wa ngozi wa kuambuk-
iza uliojitokeza pale jipu lilipokuwa.
21 Lakini ikiwa kuhani anapopachunguza
pakawa hapana nywele nyeupe ndani yake,
wala hapakuingia ndani ya ngozi, na pameanza
kupungua, basi kuhani atamtenga mtu huyo kwa
siku saba.
22 Kama unaenea kwenye ngozi, kuhani atam-
tangaza kuwa najisi; ni ugonjwa wa ngozi wa
kuambukiza.
23 Lakini ikiwa ile alama haijabadilika wala
kuenea, ni kovu tu kutokana na jipu, kuhani
atamtangaza kuwa safi.

24 “Wakati mtu ameungua kwenye ngozi yake,
pakatokea alama yenye wekundu na weupe, au
alama nyeupe ikaonekana penye nyama mbichi
pale palipoungua,
25 kuhani ataichunguza ile alama, na kama
nywele zilizo juu yake zimegeuka kuwa nyeupe,
na panaonekana kuingia ndani ya ngozi, basi
huo ni ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza ambao
umetokea katika jeraha la moto. Kuhani atam-
tangaza kuwa najisi; ni ugonjwa wa ngozi wa
kuambukiza.
26 Lakini kuhani akipachunguza na akaona
kwamba hakuna nywele nyeupe kwenye alama
ile, wala hapakuingia ndani ya ngozi, na
pamepungua, basi kuhani atamtenga kwa siku
saba.
27 Siku ya saba kuhani atamchunguza tena,
na kama unaenea kwenye ngozi, kuhani atam-
tangaza kuwa najisi; ni ugonjwa wa ngozi wa
kuambukiza.
28 Lakini, kama alama ile haikubadilika na
wala haijaenea kwenye ngozi, napo pamepun-
gua, ni uvimbe kutokana na jeraha la moto,
na kuhani atamtangaza kuwa safi; ni kovu tu
kutokana na kuungua.

29 “Ikiwa mwanaume au mwanamke ana ki-
donda juu ya kichwa au juu ya kidevu,
30 kuhani atakichunguza kile kidonda, na kama
ataona kuwa kimeingia ndani ya ngozi, na ny-
wele zilizo juu yake ni njano na nyembamba,
kuhani atamtangaza mtu huyo kuwa najisi; ni
ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza wa kichwa au
kidevu.

31 Lakini kama kuhani akichunguza aina hii ya
kidonda, kionekane kuwa hakijaingia ndani ya
ngozi, na hakuna nywele nyeusi juu yake, basi
atamtenga mtu huyo kwa siku saba.
32 Siku ya saba kuhani atachunguza kidonda
kile, na kama hakijaenea, na hakuna nywele za
manjano juu yake, wala haukuingia ndani ya
ngozi,
33 mtu huyo ni lazima anyolewe, isipokuwa ma-
hali palipo na ugonjwa, naye kuhani atamtenga
kwa siku nyingine saba.
34 Siku ya saba kuhani atachunguza tena ki-
donda kile; ikiwa hakijaenea kwenye ngozi na
hakikuingia ndani ya ngozi, kuhani atamtangaza
kuwa safi. Lazima afue nguo zake, naye atakuwa
safi.
35 Lakini ikiwa kidonda kitaenea katika ngozi
baada ya kutangazwa kuwa safi,
36 kuhani atamchunguza, na kama kidonda
kimeenea kwenye ngozi, kuhani hana haja ya
kutazama kama kuna nywele za manjano; mtu
huyo ni najisi.
37 Hata hivyo, katika uchunguzi wake akiona
hapajabadilika, na nywele nyeusi zimeota juu
yake, huyo mtu amepona. Yeye si najisi; kuhani
atamtangaza kuwa safi.

38 “Ikiwa mwanaume au mwanamke ana alama
nyeupe juu ya ngozi yake,
39 kuhani atamchunguza, na kama alama hizo
zina weupe uliofifia, ni vipele visivyo na mad-
hara vilivyojitokeza kwenye ngozi; mtu huyo ni
safi.

40 “Wakati mwanaume hana nywele naye ana upara, yeye ni safi.
41 Ikiwa hana nywele kwenye ngozi ya kichwa chake, na ana upara kwenye paji, ni safi.
42 Lakini kama ana kidonda chenye wekundu na weupe kwenye kichwa chake chenye upara, au kwenye paji la uso, ni ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza unaojitokeza kichwani au kwenye paji lake la uso.
43 Kuhani atamchunguza, na kama kidonda kilichovimba juu ya kichwa chake au kwenye paji la uso ni chekundu au cheupe kama ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza,
44 mtu huyo ni mgonjwa, na ni najisi. Kuhani atamtangaza kuwa najisi kwa sababu ya kidonda kwenye kichwa chake.

45 “Mtu mwenye ugonjwa kama huo wa kuambukiza ni lazima avae nguo zilizoraruka, awachilie nywele zake bila kuzichana, afunike sehemu ya chini ya uso wake, na apige kelele, ‘Najisi! Najisi!’
46 Kwa muda wote atakaokuwa na ugonjwa huo wa kuambukiza atabaki kuwa najisi. Ni lazima aishi peke yake; ni lazima aishi nje ya kambi.

### *Masharti kuhusu upele*

47 “Kuhusu vazi lolote lililoharibiwa na maambukizo ya ukoma, liwe ni vazi la sufu au kitani,
48 vazi lolote lililofumwa au kusokotwa la kitani au sufu, ngozi yoyote au chochote kilichotengenezwa kwa ngozi:

49 ikiwa maambukizo kwenye vazi, ngozi, au
vazi lililofumwa au kusokotwa la kitani au sufu,
au kitu chochote cha ngozi, ni rangi ya kijani au
nyekundu, huo ni ukoma unaoenea, na ni lazima
kuhani aoneshwe.
50 Kuhani atachunguza ukoma huo na
kulitenga vazi hilo kwa siku saba.
51 Siku ya saba atalichunguza, na kama ukoma
umeenea kwenye vazi, au vazi lililofumwa au kusokotwa, au ngozi, kwa vyovyote vile itumikavyo,
ni ukoma wa kuangamiza; vazi hilo ni najisi.
52 Ni lazima achome vazi hilo, liwe ni la sufu
au kitani kilichofumwa au kusokotwa, au kitu
chochote cha ngozi chenye maambukizo; kwa
kuwa ni ukoma wa kuangamiza, vazi lote ni
lazima lichomwe moto.

53 “Lakini kuhani akilichunguza na akaona
kuwa ule ukoma haujaenea kwenye vazi, au vazi
lililofumwa au kusokotwa, au kitu cha ngozi,
54 ataagiza kwamba vazi lenye maambukizo
lisafishwe. Kisha atalitenga kwa siku nyingine
saba.
55 Baada ya vazi lenye maambukizo
kusafishwa, kuhani atalichunguza, na kama
ukoma haujaonesha badiliko lolote, hata kama
haujaenea, ni najisi. Lichome kwa moto, iwe
ukoma umeenea upande mmoja au mwingine.
56 Kama kuhani ataona kuwa ile alama imefifia baada ya kuoshwa, basi atararua sehemu
iliyoambukizwa ya vazi, au ngozi, au vazi lililofumwa au kusokotwa.
57 Lakini ikijitokeza tena kwenye vazi, au vazi
lililofumwa au kusokotwa, ama kitu cha ngozi,

ule ni ukoma unaoenea; chochote chenye ukoma
ni lazima kichomwe kwa moto.
58 Vazi, au vazi lililofumwa au kusokotwa, au
kitu chochote cha ngozi, baada ya kusafishwa na
kuondolewa ukoma, ni lazima lioshwe tena, ili
liwe safi."
59 Haya ndio masharti kuhusu maambukizo ya
ukoma kwenye mavazi ya sufu au kitani, mavazi
yaliyofumwa au kusokotwa, ama kitu chochote
cha ngozi, kwa ajili ya kuvitangaza kuwa safi au
najisi.

# 14

### *Kutakasa kutoka maambukizo ya magonjwa ya ngozi*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
2 "Haya ndio masharti yanayomhusu mtu
mgonjwa wakati wa ibada yake ya utakaso,
anapoletwa kwa kuhani:
3 Kuhani ataenda kumchunguza nje ya kambi.
Kama mtu huyo atakuwa amepona ugonjwa
wake wa ngozi wa kuambukiza,
4 kuhani ataagiza vitu vifuatavyo viletwe kwa
ajili ya mtu atakayetakaswa: ndege wawili safi
walio hai, mti wa mwerezi, kitani nyekundu, na
hisopo.
5 Kisha kuhani ataagiza kwamba mmoja wa
ndege wale achinjwe kwenye chungu chenye
maji safi.
6 Kisha kuhani atamchukua ndege aliye hai
na kumtumbukiza pamoja na mti wa mwerezi,
kitani nyekundu na hisopo ndani ya damu ya
yule ndege aliyechinjiwa kwenye maji safi.

7 Atamnyunyizia yule mwenye ugonjwa wa
kuambukiza maji hayo mara saba, na kum-
tangaza kuwa safi. Kisha atamwachia yule ndege
aliye hai aende zake kwenye mashamba.
8 “Huyo mtu atakayetakaswa ni lazima afue
nguo zake, anyoe nywele zake zote, na aoge
kwa maji; ndipo atakapotakasika. Baada ya hili
anaweza kuingia kambini, lakini ni lazima akae
nje ya hema lake kwa siku saba.
9 Siku ya saba ni lazima anyoe nywele zake
zote; yaani anyoe nywele za kichwa, ndevu zake,
kope zake na nywele nyingine zote. Ni lazima
afue nguo zake, na aoge kwa maji, naye atakuwa
safi.
10 “Siku ya nane, ni lazima alete kondoo
dume wawili na kondoo jike mmoja, wote wa
mwaka mmoja na wasio na dosari, pamoja na
sehemu tatu za kumi ya efa* ya unga laini
uliochanganywa na mafuta, kwa ajili ya sadaka
ya nafaka, na logi moja† ya mafuta.
11 Kuhani anayemtangaza kuwa safi atamk-
abidhi mtu huyo atakayetakaswa pamoja na
sadaka zake zote mbele za Mwenyezi Mungu
katika ingilio la Hema la Kukutania.
12 “Kisha kuhani atamchukua mmoja wa wale
kondoo dume na kumtoa kuwa sadaka ya hatia,
pamoja na ile logi moja ya mafuta; ataviinua
mbele za Mwenyezi Mungu kuwa sadaka ya
kuinuliwa.
13 Atamchinja huyo kondoo katika mahali
patakatifu ambapo sadaka ya dhambi na ile ya

---

* **14:10** Sehemu tatu za kumi ya efa ni sawa na kilo 3. † **14:10** Kipimo cha ujazo, sawa na lita 0.3.

kuteketezwa huchinjiwa. Kama ilivyo sadaka ya
dhambi, sadaka ya hatia ni ya kuhani; ni takatifu
sana.
14 Kuhani atachukua sehemu ya damu ya
sadaka ya hatia na kuitia kwenye ncha ya sikio
la kuume la yule atakayetakaswa, kwenye kidole
gumba cha mkono wake wa kuume, na kidole
kikubwa cha mguu wake wa kuume.
15 Kisha kuhani atachukua sehemu ya ile
logi ya mafuta, ayamimine kwenye kiganja cha
mkono wake mwenyewe wa kushoto,
16 na achovye kidole chake cha shahada cha
mkono wake wa kuume kwenye mafuta yaliyo
kwenye kiganja chake, na kwa kidole hicho
anyunyize mafuta hayo mara saba mbele za
Mwenyezi Mungu.
17 Kuhani atampaka yule anayetakaswa sehemu ya mafuta yaliyobaki kiganjani kwenye
ncha ya sikio lake la kuume, kwenye kidole
gumba cha mkono wake wa kuume, na kidole
kikubwa cha mguu wake wa kuume, mahali
palepale alipompaka damu ya sadaka ya kuondoa hatia.
18 Kuhani atayapaka mafuta yaliyobaki
kwenye kiganja chake juu ya kichwa cha yule
anayetakaswa, na kufanya upatanisho kwa ajili
yake mbele za Mwenyezi Mungu.

19 “Kisha kuhani atatoa dhabihu ya sadaka ya
dhambi na kufanya upatanisho kwa ajili ya yule
atakayetakaswa kutoka unajisi wake. Baada ya
hayo, kuhani atachinja sadaka ya kuteketezwa
20 na kuitoa juu ya madhabahu, pamoja na
sadaka ya nafaka ili kumfanyia upatanisho, naye

atakuwa safi.
21 “Hata hivyo, kama ni maskini na hawezi
kupata vitu hivi, lazima achukue mwana-kondoo
wa kiume mmoja kuwa sadaka ya hatia ipate
kuinuliwa ili kumfanyia upatanisho, pamoja
na sehemu ya kumi ya efa‡ ya unga laini
uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya sadaka
ya nafaka, logi moja ya mafuta,
22 na hua wawili au makinda wawili wa
njiwa, kile atakachoweza kupata, mmoja kwa
sadaka ya dhambi, na mwingine kwa sadaka ya
kuteketezwa.
23 “Katika siku ya nane, lazima avilete vitu
hivyo kwa kuhani, kwa ajili ya kutakaswa kwake
kwenye ingilio la Hema la Kukutania mbele za
Mwenyezi Mungu.
24 Kuhani atamchukua mwana-kondoo kwa
ajili ya sadaka ya hatia, pamoja na ile logi ya
mafuta ya kuinuliwa mbele za Mwenyezi Mungu
kuwa sadaka ya kuinuliwa.
25 Atamchinja huyo mwana-kondoo kwa ajili
ya sadaka ya hatia. Kisha ataichukua sehemu
ya damu yake na kuipaka kwenye ncha ya sikio
la kuume la yule anayetakaswa, na aipake pia
kwenye kidole gumba cha mkono wa kuume wa
huyo mtu, na kidole kikubwa cha mguu wake wa
kuume.
26 Kuhani atamiminia sehemu ya mafuta
kwenye kiganja chake cha mkono wa kushoto,
27 na kwa kidole chake cha shahada cha mkono
wa kuume, atamnyunyizia yule anayetakaswa

‡ **14:21** Sehemu ya kumi ya efa ni sawa na lita 2.

yale mafuta yaliyo kwenye kiganja chake mara saba mbele za Mwenyezi Mungu.

28 Atampaka mafuta yaliyobaki kwenye kiganja chake katika sehemu zote, kama alivyompaka damu ya sadaka ya hatia: yaani kwenye ncha ya sikio la kuume la yule anayetakaswa, kwenye kidole gumba cha mkono wake wa kuume, na kidole kikubwa cha mguu wake wa kuume.

29 Kuhani atayapaka mafuta yaliyobaki katika kiganja chake kwenye kichwa cha yule anayetakaswa, na kufanya upatanisho kwa ajili yake mbele za Mwenyezi Mungu.

30 Kisha atatoa dhabihu wale hua ama makinda wa njiwa ambao yule mtu ataweza kuwapata,

31 mmoja kwa ajili ya sadaka ya dhambi, na mwingine kuwa sadaka ya kuteketezwa, pamoja na sadaka ya nafaka. Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho mbele za Mwenyezi Mungu kwa ajili ya yule anayetakaswa."

32 Haya ndio masharti kwa mtu yeyote mwenye ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza, na ambaye hana uwezo wa kutoa sadaka za kawaida kwa ajili ya kutakaswa kwake.

### *Kutakaswa upele*

33 Mwenyezi Mungu akawaambia Musa na Haruni,

34 "Mtakapoingia katika nchi ya Kanaani ninayowapa kuwa milki yenu, nami nikaweka ukoma§ unaoenea kwenye nyumba katika nchi ile,

§ **14:34** ugonjwa wowote wa ngozi wa kuambukiza; pia hutumiwa kwa maambukizi kwenye mawe au matofali ya nyumba

35 ni lazima mwenye nyumba hiyo
akamwambie kuhani, ‘Nimeona kitu fulani
kinachofanana na ukoma kwenye nyumba
yangu.’
36 Kuhani ataagiza vitu vyote vitolewe ndani ya
nyumba, kabla hajaenda kuchunguza kama ina
ukoma huo, ili kitu chochote ndani ya nyumba
kisitangazwe kuwa najisi. Baada ya hili, kuhani
ataingia ndani na kuikagua hiyo nyumba.
37 Atachunguza ukoma huo katika kuta za
nyumba hiyo, nazo kama zina rangi ya kijani
kibichi au wekundu, na kuna mibonyeo ndani ya
ukuta,
38 kuhani atatoka na kufunga mlango wa
nyumba hiyo kwa siku saba.
39 Siku ya saba, kuhani atarudi kuikagua
nyumba. Kama ukoma umeenea juu ya kuta,
40 ataagiza kwamba mawe yote yaliyoambuk-
izwa yaondolewe na kutupwa katika eneo lililo
najisi nje ya mji.
41 Kuta zote za ndani ya nyumba hiyo ni lazima
zikwanguliwe, na kifusi chake kitupwe mahali
najisi nje ya mji.
42 Kisha watachukua mawe mengine na ku-
jenga palipobomolewa kwa udongo mpya wa
mfinyanzi, na wapake nyumba hiyo chokaa.

43 “Ikiwa ukoma huo utatokea tena ndani ya
ile nyumba baada ya mawe kuondolewa, na
nyumba kukwanguliwa na kupakwa chokaa,
44 kuhani ataenda kuikagua, na kama ukoma
umeenea ndani ya nyumba, basi ni ukoma unao-
haribu; nyumba hiyo ni najisi.

45 Ni lazima ibomolewe: mawe yake, mbao na chokaa yote; vyote vikatupwe nje ya mji mahali palipo najisi.
46 “Yeyote atakayeingia katika nyumba hiyo ikiwa imefungwa, atakuwa najisi hadi jioni.
47 Yeyote atakayelala au kula ndani ya nyumba hiyo ni lazima afue nguo zake.
48 “Lakini ikiwa kuhani atakuja kuikagua na kukuta kuwa ukoma haujaenea tena baada ya nyumba kupakwa chokaa, ataitangaza nyumba ile kuwa safi, kwa sababu ukoma umekwisha.
49 Ili kuitakasa nyumba hiyo, mwenye nyumba ataleta ndege wawili, mti wa mwerezi, kitani nyekundu na hisopo.
50 Atamchinja mmoja wa wale ndege kwenye chungu chenye maji safi.
51 Kisha atachukua mti wa mwerezi, hisopo, kitani nyekundu na ndege aliye hai, na kuvitumbukiza ndani ya damu ya ndege aliyechinjwa pamoja na maji safi, na kuinyunyizia nyumba ile mara saba.
52 Ataitakasa nyumba kwa damu ya yule ndege, maji safi, ndege aliye hai, mti wa mwerezi, hisopo na uzi mwekundu.
53 Kisha atamwachia yule ndege aliye hai huru mashambani nje ya mji. Kwa njia hii atafanya upatanisho kwa ajili ya nyumba ile, nayo itakuwa safi.”
54 Haya ndio masharti kuhusu aina yoyote ya ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza*, kidonda

* **14:54** yaani *ukoma*; ni neno lililotumika kueleza magonjwa mbalimbali ya ngozi, ambayo si lazima yawe ni ukoma halisi

chochote,
55 ukoma katika vazi au ndani ya nyumba,
56 kwa uvimbe, upele, au alama nyeupe katika ngozi,
57 kupambanua wakati kitu fulani ni safi au najisi.

Haya ndio masharti kuhusu magonjwa ya ngozi ya kuambukiza na ukoma.

# 15

### *Kutokwa na usaha usababishao unajisi*

1 Mwenyezi Mungu akawaambia Musa na Haruni,
2 "Semeni na Waisraeli mwaambie: 'Mtu yeyote anapotokwa na usaha mwilini, usaha huo ni najisi.
3 Iwe unaendelea kutiririka kutoka mwilini mwake au umeziba, utamfanya najisi. Hivi ndivyo usaha wake utakavyomletea unajisi:
4 " 'Kitanda chochote atakacholalia mtu mwenye kutokwa na usaha kitakuwa najisi, na chochote atakachokalia kitakuwa najisi.
5 Yeyote atakayegusa kitanda chake ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi hadi jioni.
6 Yeyote atakayeketi juu ya kitu chochote alichokalia mwenye kutokwa na usaha, ni lazima afue nguo zake, na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi hadi jioni.
7 " 'Yeyote atakayemgusa mtu mwenye kutokwa na usaha, ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi hadi jioni.

8 “ ‘Ikiwa mtu mwenye kutokwa na usaha
atamtemea mate mtu ambaye ni safi, mtu huyo
ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye
atakuwa najisi hadi jioni.

9 “ ‘Kila tandiko ambalo mtu huyo atalikalia
wakati wa kupanda mnyama litakuwa najisi,
10 na yeyote atakayegusa kitu chochote ali-
chokuwa amekalia atakuwa najisi hadi jioni. Yey-
ote atakayeinua vitu hivyo ni lazima afue nguo
zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi hadi
jioni.

11 “ ‘Yeyote atakayeguswa na mtu anayetokwa
na usaha bila kunawa mikono yake kwa maji, ni
lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye
atakuwa najisi hadi jioni.

12 “ ‘Chungu cha udongo kitakachoguswa na
mtu huyo ni lazima kivunjwe, na kifaa chochote
cha mbao kitaoshwa kwa maji.

13 “ ‘Mtu atakapotakasika kutoka usaha wake,
atahesabu siku saba kwa utakaso wake. Ni
lazima afue nguo zake na aoge kwa maji safi,
naye atatakasika.
14 Siku ya nane, atachukua hua wawili
au makinda wawili wa njiwa, aje mbele za
Mwenyezi Mungu kwenye ingilio la Hema la
Kukutania, na kumpa kuhani.
15 Kuhani atawatoa dhabihu, mmoja kwa ajili
ya sadaka ya dhambi, na huyo mwingine kwa
ajili ya sadaka ya kuteketezwa. Kwa njia hii
atafanya upatanisho mbele za Mwenyezi Mungu
kwa ajili ya huyo mtu kwa sababu ya kutokwa
usaha kwake.

16 “ ‘Mtu akitokwa na shahawa, ni lazima aoge mwili mzima kwa maji, na atakuwa najisi hadi jioni.
17 Vazi lolote ama ngozi yoyote yenye shahawa juu yake ni lazima ioshwe kwa maji, na itakuwa najisi hadi jioni.
18 Ikiwa mtu atalala na mwanamke, na kukawa na kutoka kwa shahawa, ni lazima wote waoge kwa maji, nao watakuwa najisi hadi jioni.
19 “ ‘Ikiwa mwanamke atatokwa na damu ya kawaida ya mwezi, atakuwa najisi kwa siku saba, na yeyote atakayemgusa atakuwa najisi hadi jioni.
20 “ ‘Chochote atakacholalia wakati wake wa hedhi kitakuwa najisi, na chochote atakachokikalia kitakuwa najisi.
21 Yeyote atakayegusa kitanda chake ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi hadi jioni.
22 Yeyote atakayegusa chochote atakachokalia ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi hadi jioni.
23 Kiwe ni kitanda ama chochote alichokuwa amekikalia, ikiwa mtu yeyote atakigusa, atakuwa najisi hadi jioni.
24 “ ‘Ikiwa mwanaume atalala naye na ile damu ya mwezi ikamgusa, atakuwa najisi kwa siku saba; kitanda chochote atakachokilalia huyo mwanaume kitakuwa najisi.
25 “ ‘Ikiwa mwanamke atatokwa na damu kwa siku nyingi zaidi ya siku zake za mwezi, au amekuwa na damu inayoendelea zaidi ya kipindi chake, atakuwa najisi kwa kipindi chote cha

shida hiyo, kama ilivyokuwa katika siku za hedhi
yake.
26 Kitanda chochote atakachokilalia huyo
mwanamke wakati anaendelea kutokwa na
damu kitakuwa najisi, kama kilivyokuwa kitanda
chake wakati wa siku zake za hedhi, na chochote
atakachokalia kitakuwa najisi, kama wakati
wake wa hedhi.
27 Yeyote agusaye vitu hivyo atakuwa najisi; ni
lazima afue nguo zake na kuoga kwa maji, naye
atakuwa najisi hadi jioni.
28 " 'Atakapotakasika kutoka hedhi yake, ni
lazima ahesabu siku saba, na baada ya hapo
atakuwa ametakasika kabisa.
29 Siku ya nane ni lazima achukue hua waw-
ili au makinda wawili wa njiwa, na kumletea
kuhani kwenye mlango wa Hema la Kukutania.
30 Kuhani atatoa dhabihu, mmoja kwa ajili ya
sadaka ya dhambi, na huyo mwingine kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa. Kwa njia hii, atafanya
upatanisho kwa ajili yake mbele za Mwenyezi
Mungu kwa sababu ya unajisi wa kutokwa damu
kwake.
31 " 'Ni lazima uwatenge Waisraeli kutokana
na vitu ambavyo vinawafanya najisi, ili wasife
katika unajisi wao kwa kunajisi makao yangu*
yaliyo katikati yao.' "
32 Haya ni masharti kwa ajili ya mtu
mwenye kutokwa na usaha, kwa ajili ya yeyote
atakayetokwa na shahawa,
33 kwa ajili ya mwanamke katika siku zake za
hedhi, kwa ajili ya mwanaume au mwanamke

* **15:31** yaani *maskani ya Mungu*

atokwaye na usaha, na kwa ajili ya mwanaume alalaye na mwanamke ambaye ni najisi.

# 16

## *Siku ya Upatanisho*

1 Mwenyezi Mungu akasema na Musa baada ya
kifo cha wale wana wawili wa Haruni waliokufa
walipokaribia mbele za Mwenyezi Mungu.
2 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa:
“Mwambie ndugu yako Haruni asije wakati
wowote anaotaka ndani ya Patakatifu pa
Patakatifu, nyuma ya pazia pale mbele ya kiti
cha rehema kile kilicho juu ya Sanduku la Agano,
la sivyo atakufa, kwa sababu huwa ninatokea
ndani ya wingu juu ya kile kiti cha rehema.

3 “Hivi ndivyo Haruni atakavyoingia katika
Mahali Patakatifu: atachukua fahali mchanga
kwa ajili ya sadaka ya dhambi, na kondoo dume
kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa.
4 Atavaa koti takatifu la kitani, pamoja na nguo
za ndani za kitani; atafunga mshipi wa kitani
kiunoni, na kuvaa kilemba cha kitani. Haya ni
mavazi matakatifu, kwa hiyo ni lazima aoge kwa
maji kabla ya kuyavaa mavazi hayo.
5 Atachukua beberu wawili kutoka kwa
jumuiya ya Israeli kwa ajili ya sadaka ya
dhambi, na kondoo dume kwa ajili ya sadaka
ya kuteketezwa.

6 “Haruni atamtoa huyo fahali kwa ajili ya
sadaka yake ya dhambi ili afanye upatanisho kwa
ajili yake mwenyewe na nyumba yake.

7 Kisha atawachukua wale beberu wawili na
kuwaleta mbele za Mwenyezi Mungu kwenye
ingilio la Hema la Kukutania.
8 Haruni atapiga kura kwa ajili ya hao mbuzi
wawili, mmoja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na
mwingine kwa ajili ya kubebeshwa dhambi[*] za
Israeli.
9 Haruni atamleta yule mbuzi ambaye kura
ya Mwenyezi Mungu imemwangukia na kumtoa
dhabihu kwa ajili ya sadaka ya dhambi.
10 Lakini mbuzi aliyechaguliwa kwa kura kuwa
wa kubebeshwa dhambi atatolewa akiwa hai
mbele za Mwenyezi Mungu, atumike kwa ku-
fanya upatanisho kwa kumwacha aende jang-
wani akiwa amebebeshwa dhambi.
11 “Haruni atamleta yule fahali kwa ajili ya
sadaka ya dhambi yake mwenyewe, ili kufanya
upatanisho kwa ajili yake na nyumba yake, naye
atamchinja huyo fahali kwa ajili ya sadaka ya
dhambi yake mwenyewe.
12 Atachukua chetezo kilichojaa makaa
yanayowaka kutoka madhabahuni mbele za
Mwenyezi Mungu, na konzi mbili za uvumba
laini uliosagwa vizuri wenye harufu, na
kuvipeleka nyuma ya pazia.
13 Ataweka uvumba juu ya moto mbele za
Mwenyezi Mungu, na moshi wa uvumba uta-
funika kile kiti cha rehema kilicho juu ya
Ushuhuda, ili asife.
14 Atachukua sehemu ya damu ya fahali, na
kwa kidole chake atanyunyiza sehemu ya mbele

[*] **16:8** yaani *Azazeli,* maana yake *mbuzi wa ondoleo la dhambi*; pia 16:10, 26

ya kiti cha rehema; kisha atanyunyiza sehemu ya hiyo damu kwa kidole chake mara saba mbele ya kiti cha rehema.

15 “Kisha atamchinja mbuzi wa sadaka ya dhambi kwa ajili ya watu, na kuichukua damu yake nyuma ya pazia, na aifanyie kama alivyofanya kwa damu ya fahali: Atanyunyiza juu ya kiti cha rehema na mbele yake.

16 Kwa njia hii atafanya upatanisho kwa ajili ya Patakatifu pa Patakatifu kwa sababu ya unajisi na uasi wa Waisraeli, kwa dhambi zao zozote. Atafanya hivyo kwa ajili ya Hema la Kukutania, ambalo liko miongoni mwao katikati ya unajisi wao.

17 Mtu yeyote haruhusiwi kuwa ndani ya Hema la Kukutania, kuanzia wakati Haruni anapoingia kufanya upatanisho katika Patakatifu pa Patakatifu, hadi atakapotoka nje, baada ya kujifanyia upatanisho yeye mwenyewe na nyumba yake, pamoja na jumuiya yote ya Israeli.

18 “Kisha atatoka aje kwenye madhabahu yaliyo mbele za Mwenyezi Mungu na kufanya upatanisho kwa ajili yake. Atachukua sehemu ya damu ya fahali na sehemu ya damu ya mbuzi, na kuiweka kwenye pembe za madhabahu.

19 Atanyunyiza sehemu ya hiyo damu juu ya madhabahu kwa kidole chake mara saba, ili kuitakasa na kuiweka wakfu kutokana na unajisi wa Waisraeli.

20 “Haruni atakapokuwa amemaliza kufanya upatanisho kwa ajili ya Patakatifu pa Patakatifu, Hema la Kukutania na madhabahu, atamleta mbele yule mbuzi aliye hai.

21 Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha mbuzi aliye hai, na kuungama juu yake uovu wote na uasi wa Waisraeli, yaani dhambi zao zote, ili kuziweka juu ya kichwa cha huyo mbuzi. Atamwachia huyo mbuzi akimbilie jangwani kwa uangalizi wa mtu aliyepewa wajibu huo.

22 Yule mbuzi atachukua juu yake dhambi zao zote hadi mahali pasipo na watu; naye yule mtu atamwachia akimbilie jangwani.

23 “Kisha Haruni ataenda ndani ya Hema la Kukutania na kuvua yale mavazi ya kitani aliyoyavaa kabla ya kuingia katika Patakatifu pa Patakatifu, naye atayaacha pale.

24 Ataoga kwa maji katika mahali patakatifu na kuvaa mavazi yake ya kawaida. Kisha atatoka na kutoa dhabihu ya sadaka ya kuteketezwa kwa ajili yake na sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya watu, ili kufanya upatanisho kwa ajili yake mwenyewe, na kwa ajili ya watu.

25 Pia atachoma mafuta ya mnyama wa sadaka ya dhambi juu ya madhabahu.

26 “Yule mtu anayemwachia yule mbuzi wa kubebeshwa dhambi ni lazima afue nguo zake na kuoga kwa maji; baadaye anaweza kuingia kambini.

27 Yule fahali na mbuzi waliotolewa kwa ajili ya sadaka za dhambi, ambao damu yao ilikuwa imeletwa Patakatifu pa Patakatifu kwa ajili ya kufanya upatanisho, ni lazima watolewe nje ya kambi. Ngozi zao, nyama, na matumbo vitateketezwa kwa moto.

28 Mtu atakayevichoma ni lazima afue nguo
zake na aoge kwa maji; baadaye ataweza kuingia
kambini.
29 “Hili litakuwa agizo la kudumu kwa ajili
yenu: Katika siku ya kumi ya mwezi wa saba ni
lazima mfunge, wala msifanye kazi yoyote, iwe
mzawa au mgeni anayeishi miongoni mwenu,
30 kwa sababu siku hii upatanisho utafanyika
kwa ajili yenu ili kuwatakasa. Kisha mtakuwa
safi mbele za Mwenyezi Mungu kutokana na
dhambi zenu zote.
31 Ni Sabato ya mapumziko, na lazima mfunge;
ni agizo la kudumu.
32 Kuhani ambaye amepakwa mafuta na
kuwekwa wakfu ili kuingia mahali pa baba
yake kama kuhani mkuu atafanya upatanisho.
Atavaa mavazi matakatifu ya kitani,
33 na kufanya upatanisho kwa ajili ya Patakat-
ifu pa Patakatifu, Hema la Kukutania na mad-
habahu, na pia kwa ajili ya makuhani, pamoja na
jumuiya yote ya watu.
34 “Hili litakuwa agizo la kudumu kwa ajili
yenu: Upatanisho utafanywa mara moja tu kwa
mwaka kwa ajili ya dhambi zote za Waisraeli.”

Ndivyo ilivyofanyika, kama vile Mwenyezi Mungu alivyomwamuru Musa.

# 17

### *Kunywa damu kunakatazwa*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,

2 “Sema na Haruni na wanawe, pamoja na
Waisraeli wote, uwaambie: ‘Hili ndilo Mwenyezi
Mungu aliloagiza:
3 Mwisraeli yeyote atakayetoa dhabihu ya
ng’ombe, mwana-kondoo au mbuzi ndani ya
kambi au nje yake,
4 badala ya kuileta kwenye ingilio la Hema la
Kukutania ili kuileta kama sadaka kwa Mwenyezi
Mungu mbele ya Maskani ya Mwenyezi Mungu,
mtu huyo atahesabiwa kuwa na hatia ya
kumwaga damu; amemwaga damu, na ni lazima
akatiliwe mbali na watu wake.
5 Hii ni ili Waisraeli wamletee Mwenyezi
Mungu dhabihu wanazozifanya sasa mahali pa
wazi mashambani. Ni lazima wazilete kwa
makuhani, yaani kwa Mwenyezi Mungu, katika
ingilio la Hema la Kukutania, na kutoa dhabihu
kuwa sadaka za amani.
6 Kuhani atanyunyiza damu kwenye mad-
habahu ya Mwenyezi Mungu katika ingilio la
Hema la Kukutania, na kuyateketeza mafuta ya
hiyo dhabihu kuwa harufu nzuri ya kumpendeza
Mwenyezi Mungu.
7 Kamwe wasitoe tena dhabihu zao kwa
sanamu za mbuzi ambazo wamekuwa wakiji-
fanyia nazo ukahaba. Hili litakuwa agizo la
kudumu kwao na kwa vizazi vijavyo.’

8 “Waambie: ‘Mwisraeli yeyote au mgeni yeyote
anayeishi miongoni mwao atakayetoa sadaka ya
kuteketezwa au dhabihu
9 bila kuileta kwenye ingilio la Hema la Kukuta-
nia ili kutoa dhabihu kwa Mwenyezi Mungu, mtu
huyo ni lazima akatiliwe mbali na watu wake.

10 “ ‘Mwisraeli yeyote au mgeni anayeishi mion-
goni mwao ambaye atakula damu yoyote, ni-
takuwa kinyume chake, na nitamkatilia mbali na
watu wake.
11 Kwa kuwa uhai wa kiumbe uko ndani ya
damu, nami nimewapa hiyo damu ili mfanyie
upatanisho kwa ajili yenu wenyewe juu ya mad-
habahu; damu ndiyo ifanyayo upatanisho kwa
ajili ya maisha ya mtu.
12 Kwa hiyo, ninawaambia Waisraeli, “Hakuna
hata mmoja wenu anayeruhusiwa kula damu,
wala mgeni anayeishi miongoni mwenu
haruhusiwi kula damu.”
13 “ ‘Mwisraeli yeyote au mgeni anayeishi mion-
goni mwenu ambaye atamwinda mnyama au
ndege anayeruhusiwa kuliwa ni lazima aimwage
damu na kuifunika kwa udongo,
14 kwa sababu uhai wa kila kiumbe ni damu
yake. Ndiyo sababu nimewaambia Waisraeli,
“Kamwe msile damu ya kiumbe chochote, kwa
sababu uhai wa kila kiumbe ni damu yake; yey-
ote atakayekula damu lazima akatiliwe mbali.”
15 “ ‘Mtu yeyote, awe mzawa au mgeni, am-
baye atakula mzoga wa kitu chochote ama kili-
chouawa na wanyama mwitu ni lazima afue
nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi
hadi jioni; kisha atakuwa ametakaswa.
16 Lakini kama hakufua nguo zake na kuoga,
atakuwa na hatia kwa kosa hilo.’ ”

# 18

*Uhusiano wa kukutana kimwili kinyume cha Torati*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
2 “Sema na Waisraeli uwaambie: ‘Mimi ndimi
Mwenyezi Mungu, Mungu wenu.
3 Msifanye kama wafanyavyo huko Misri, ma-
hali mlipokuwa mnaishi, wala msifanye kama
wanavyofanya katika nchi ya Kanaani, mahali
ninapowapeleka. Msifuate matendo yao.
4 Ni lazima mzitii sheria zangu, na mwe
waangalifu kuzifuata amri zangu. Mimi ndimi
Mwenyezi Mungu, Mungu wenu.
5 Zishikeni amri zangu na sheria zangu, kwa
maana mtu anayezitii ataishi kwa hizo. Mimi
ndimi Mwenyezi Mungu.
6 “ ‘Hakuna mtu yeyote atakayemsogelea ndugu
wa karibu ili kukutana naye kimwili. Mimi ndimi
Mwenyezi Mungu.
7 “ ‘Usimvunjie heshima baba yako kwa kuku-
tana kimwili na mama yako. Yeye ni mama yako;
usiwe na mahusiano kama hayo naye.
8 “ ‘Usikutane kimwili na mke wa baba yako;
hiyo itamvunjia heshima baba yako.
9 “ ‘Usikutane kimwili na dada yako, wala binti
ya baba yako, au binti ya mama yako, awe ameza-
liwa katika nyumba hiyo au mahali pengine.
10 “ ‘Usikutane kimwili na binti ya mwanao ama
binti ya binti yako; utajivunjia heshima.
11 “ ‘Usikutane kimwili na binti ya mke wa baba
yako, aliyezaliwa na baba yako; huyo ni dada
yako.
12 “ ‘Usikutane kimwili na dada wa baba yako;
ni ndugu wa karibu wa baba yako.
13 “ ‘Usikutane kimwili na dada wa mama yako,
kwa sababu ni ndugu wa mama yako wa karibu.

14 “ ‘Usimvunjie heshima ndugu wa baba yako,
kwa kukutana kimwili na mke wake; yeye ni
shangazi yako.

15 “ ‘Usikutane kimwili na mkwe wako, yeye
ni mke wa mwanao; usiwe na mahusiano kama
hayo naye.

16 “ ‘Usikutane kimwili na mke wa kaka yako;
utamvunjia heshima kaka yako.

17 “ ‘Usikutane kimwili na mwanamke kisha
na binti yake. Usikutane kimwili na binti ya
mwanawe au binti ya binti yake; hao ni ndugu
zake wa karibu. Huo ni uovu.

18 “ ‘Usimchukue dada wa mke wako kuwa mke
mwenza, na kukutana naye kimwili wakati bado
mke wako anaishi.

19 “ ‘Usimsogelee mwanamke ili kukutana naye
kimwili wakati wa unajisi wa siku zake za mwezi.

20 “ ‘Usikutane kimwili na mke wa jirani yako
na kujitia naye unajisi.

21 “ ‘Usimtoe kafara mtoto wako yeyote kwa
Moleki, kwani hutalinajisi kamwe jina la Mungu
wako. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.

22 “ ‘Usikutane kimwili na mwanaume
vile mwanaume anavyokutana kimwili na
mwanamke; hilo ni chukizo.

23 “ ‘Usikutane kimwili na mnyama na kuji-
tia unajisi kwake. Mwanamke asijipeleke kwa
mnyama ili kukutana naye kimwili; huo ni upo-
tovu.

24 “ ‘Msijitie unajisi kwa njia yoyote katika hizi,
kwa sababu hivi ndivyo mataifa nitakayoya-
fukuza mbele yenu yalivyojitia unajisi.

25 Hata nchi ilitiwa unajisi, hivyo nikaiadhibu kwa dhambi zake, nayo nchi ikawatapika wakazi wake.
26 Lakini ni lazima mzitunze amri zangu na sheria zangu. Wazawa na wageni wanaoishi miongoni mwenu kamwe wasifanye mambo yoyote ya machukizo haya,
27 kwa kuwa mambo haya yote yalifanywa na watu walioishi katika nchi hii kabla yenu, na nchi ikawa najisi.
28 Mkiinajisi nchi, itawatapika kama ilivyowatapika mataifa yaliyowatangulia.

29 " 'Kila mtu atakayefanya mojawapo ya machukizo haya, watu hao ni lazima wakatiliwe mbali na watu wao.
30 Shikeni maagizo yangu, wala msifuate desturi za machukizo yoyote yaliyofanywa kabla hamjafika katika nchi hii, na kujitia unajisi kwa hayo. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu.' "

# 19

*Sheria mbalimbali*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
2 "Sema na kusanyiko lote la Waisraeli, uwaambie: 'Kuweni watakatifu, kwa kuwa mimi, Mwenyezi Mungu, Mungu wenu, ni mtakatifu.

3 " 'Kila mmoja wenu ni lazima amheshimu mama yake na baba yake, na pia ni lazima kuzishika Sabato zangu. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu.

4 “ ‘Msiabudu sanamu, wala msijitengenezee
miungu ya kusubu. Mimi ndimi Mwenyezi
Mungu, Mungu wenu.

5 “ ‘Mnapotoa dhabihu ya sadaka ya amani kwa
Mwenyezi Mungu, toeni kwa namna ambayo
itakubaliwa kwa niaba yenu.
6 Sadaka hiyo italiwa siku hiyo hiyo mnayoitoa,
au kesho yake; chochote kitakachobaki hadi siku
ya tatu lazima kiteketezwe kwa moto.
7 Kama sehemu yoyote ya sadaka hiyo italiwa
siku ya tatu, itakuwa si safi, nayo haitakubaliwa.
8 Yeyote atakayekula atawajibishwa, kwa
sababu amenajisi kitu kilicho kitakatifu kwa
Mwenyezi Mungu; mtu huyo lazima akatiliwe
mbali na watu wake.
9 “ ‘Unapovuna mavuno ya nchi yako, usivune
hadi kwenye mipaka ya shamba lako, wala usiku-
sanye mabaki ya mavuno yako.
10 Usirudi mara ya pili katika shamba lako
la mizabibu, wala usiokote zabibu zilizoanguka
chini. Ziache kwa ajili ya maskini na mgeni.
Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wako.

11 “ ‘Usiibe.

“ ‘Usiseme uongo.

“ ‘Msidanganyane.

12 “ ‘Usiape kwa uongo kwa Jina langu, na hivyo
kulinajisi jina la Mungu wako. Mimi ndimi
Mwenyezi Mungu.

13 “ ‘Usimdhulumu wala kumwibia jirani yako.

“ ‘Usishikilie mshahara wa kibarua usiku kucha
hadi asubuhi.

14 “ ‘Usimlaani kiziwi, wala usiweke kikwazo
mbele ya kipofu, lakini umche Mungu wako.
Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.
15 “ ‘Usipotoshe haki; usioneshe kumpendelea
maskini, wala upendeleo kwa mwenye cheo, bali
mwamulie jirani yako kwa haki.
16 “ ‘Usieneze uchochezi miongoni mwa watu
wako.

“ ‘Usifanye kitu chochote kile kinachohatarisha maisha ya jirani yako. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.

17 “ ‘Usimchukie ndugu yako moyoni mwako.
Karipia jirani yako kwa uwazi ili usishiriki hatia
yake.
18 “ ‘Usijilipizie kisasi wala kuwa na kinyongo
dhidi ya mmoja wa jamaa yako, lakini mpende
jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.
Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.
19 “ ‘Mtazishika amri zangu.

“ ‘Usiwaache mifugo wako wakazaana na wa aina tofauti.

“ ‘Usipande mbegu za aina mbili katika shamba lako.

“ ‘Usivae vazi lililofumwa kwa nyuzi za aina mbili tofauti.

20 “ ‘Kama mwanaume anakutana kimwili na
mjakazi aliyeposwa na mwanaume mwingine,
ambaye hajakombolewa wala hajapewa uhuru,
lazima iwepo adhabu inayofaa. Hata hivyo
hawatauawa, kwa sababu msichana alikuwa
bado hajaachwa huru.
21 Lakini huyo mtu lazima alete kondoo dume
kwenye ingilio la Hema la Kukutania kwa ajili ya
sadaka ya hatia kwa Mwenyezi Mungu.

22 Kupitia kwa huyo kondoo dume wa sadaka ya hatia, kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake mbele za Mwenyezi Mungu kwa ajili ya dhambi aliyotenda, naye atasamehewa dhambi yake.

23 " 'Mtakapoingia katika hiyo nchi na kupanda aina yoyote ya mti wa matunda, hesabuni matunda yake kama yaliyokatazwa. Kwa miaka mitatu mtayahesabu kwamba yamekatazwa; hayaruhusiwi kuliwa.

24 Katika mwaka wa nne matunda yote ya mti huo yatakuwa matakatifu, sadaka ya sifa kwa Mwenyezi Mungu.

25 Bali katika mwaka wa tano mnaweza kula matunda ya mti huo. Kwa njia hii mavuno yenu yataongezewa. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wako.

26 " 'Msile nyama yoyote yenye damu ndani yake.

" 'Msifanye uaguzi wala uchawi.

27 " 'Msikate nywele za kichwa denge, wala kunyoa pembe za ndevu zenu.

28 " 'Msichanje chale miili yenu kwa ajili ya mfu, wala msijichore alama juu ya miili yenu. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.

29 " 'Usimdhalilishe binti yako kwa kumfanya kahaba, la sivyo nchi itageukia ukahaba na kujaa uovu.

30 " 'Shika Sabato zangu na kuheshimu mahali pangu patakatifu. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.

31 " 'Msiende kwa waaguzi, wala msitafute wapunga pepo, kwa maana watawanajisi. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wako.

32 “ ‘Ukiwa mbele ya mzee, simama ili kuonesha
heshima kwa wazee, nawe umche Mungu wako.
Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.
33 “ ‘Wakati mgeni anaishi pamoja nawe katika
nchi yako, usimnyanyase.
34 Mgeni anayeishi pamoja nawe ni lazima
umtendee kama mmoja wa wazawa wa nchi
yako. Mpende kama unavyojipenda mwenyewe,
kwa maana ulikuwa mgeni katika nchi ya Misri.
Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wako.
35 “ ‘Usitumie vipimo vya udanganyifu un-
apopima urefu, kupima uzito, wala kupima
wingi.
36 Tumia mizani halali, mawe ya kupimia uzito
halali, efa* halali, na hini† halali. Mimi ndimi
Mwenyezi Mungu, Mungu wako, ambaye aliku-
toa katika nchi ya Misri.
37 “ ‘Shika amri zangu zote na sheria zangu zote,
nawe uzifuate. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.’ ”

# 20

## *Adhabu kwa ajili ya dhambi*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
2 “Waambie Waisraeli: ‘Mwisraeli yeyote au
mgeni anayeishi Israeli atakayemtoa kafara
mtoto wake yeyote kwa Moleki lazima auawe.
Watu wa jumuiya hiyo watampiga kwa mawe.
3 Mimi nitauelekeza uso wangu dhidi ya mtu
huyo, nami nitamkatilia mbali na watu wake.

---

* **19:36** Efa kilikuwa kipimo cha vitu vikavu. † **19:36** Hini kilikuwa kipimo cha vitu vimiminika.

Kwa maana kwa kumtoa kafara mmoja wa watoto wake kwa Moleki, amenajisi madhabahu yangu na kulinajisi Jina langu takatifu.
4 Ikiwa watu wa jumuiya watafumba macho yao wakati mtu huyo anapomtoa kafara mmoja wa watoto wake kwa Moleki, nao wakaacha kumuua,
5 mimi nitauelekeza uso wangu dhidi ya mtu huyo pamoja na jamaa yake, nami nitawakatilia mbali yeye na watu wote waliofanya ukahaba na Moleki.
6 “ ‘Mimi nitauelekeza uso wangu dhidi ya mtu anayeenda kwa waaguzi na wenye pepo, na hivyo kujifanyia ukahaba kwa kuwafuata, nami nitamkatilia mbali na watu wake.
7 “ ‘Jitakaseni basi, nanyi kuweni watakatifu, kwa sababu mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu.
8 Shikeni amri zangu na kuzifuata. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, niwafanyaye ninyi watakatifu.
9 “ ‘Ikiwa mtu yeyote atamlaani baba yake au mama yake, lazima auawe. Amemlaani baba yake au mama yake, nayo damu yake itakuwa juu ya kichwa chake mwenyewe.
10 “ ‘Ikiwa mtu atazini na mke wa mtu mwingine, yaani mke wa jirani yake, wazinzi hao wawili lazima wauawe.
11 “ ‘Kama mtu atakutana kimwili na mke wa baba yake, hakumheshimu baba yake. Mwanaume huyo na mwanamke huyo wote wauawe; damu yao itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.

12 “ ‘Ikiwa mtu atakutana kimwili na mke wa mwanawe, lazima wote wawili wauawe. Walichokifanya ni upotovu; damu yao itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.

13 “ ‘Kama mwanaume akikutana kimwili na mwanaume mwenzake kama vile mwanaume afanyavyo na mwanamke, wanaume hao wawili wamefanya lililo chukizo sana. Lazima wauawe; nayo damu yao itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.

14 “ ‘Ikiwa mwanaume ataoa binti pamoja na mama yake, huo ni uovu. Wote watatu ni lazima wachomwe moto, ili pasiwepo na uovu kati yenu.

15 “ ‘Kama mwanaume akikutana kimwili na mnyama, ni lazima auawe, na pia ni lazima mnyama huyo auawe.

16 “ ‘Kama mwanamke atamsogelea mnyama kukutana naye kimwili, muueni mwanamke huyo pamoja na mnyama pia. Lazima wauawe; damu yao itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.

17 “ ‘Ikiwa mtu atamwoa dada yake, binti aliyezaliwa na baba yake au mama yake, nao wakakutana kimwili, ni aibu. Lazima wakatiliwe mbali machoni pa watu wao. Huyo mwanaume amemwaibisha dada yake, hivyo atawajibika kwa ajili ya uovu huo.

18 “ ‘Ikiwa mwanaume atakutana kimwili na mwanamke aliye katika hedhi yake, amefunua mtiririko wa hedhi yake, naye huyo mwanamke amejifunua uchi wake. Wote wawili lazima wakatiliwe mbali na watu wao.

19 “ ‘Usikutane kimwili na dada wa mama yako wala wa baba yako, kwa maana hilo

litamwaibisha jamaa wa karibu; ninyi wawili mtawajibika kwa ajili ya uovu huo.

20 " 'Ikiwa mwanaume atakutana kimwili na shangazi yake, amemwaibisha mjomba wake. Nao watawajibika kwa ajili ya uovu huo; watakufa bila kuzaa mtoto.
21 " 'Ikiwa mwanaume ataoa mke wa ndugu yake, hili ni tendo chafu; amemwaibisha ndugu yake. Nao hawatazaa mtoto.

22 " 'Zishikeni amri na sheria zangu zote na kuzifuata, ili nchi ninayowaleta kuishi isiwatapike.
23 Kamwe msiishi kwa kufuata desturi za mataifa nitakayoyafukuza mbele yenu. Kwa sababu walifanya mambo haya yote, nilichukizwa sana nao.
24 Lakini niliwaambia ninyi, "Mtaimiliki nchi yao; nitawapa ninyi kuwa urithi, nchi inayotiririka maziwa na asali." Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu, ambaye amewatenga kutoka mataifa.

25 " 'Kwa hiyo, ninyi lazima mweze kutofautisha kati ya wanyama walio safi na wasio safi, pia kati ya ndege wasio safi na walio safi. Msijitie unajisi kutokana na mnyama yeyote, au ndege, wala kiumbe chochote kinachotambaa juu ya ardhi, ambavyo nimevitenga kuwa najisi kwa ajili yenu.
26 Mtakuwa watakatifu kwangu, kwa sababu Mimi, Mwenyezi Mungu, ni mtakatifu, nami nimewatenga kutoka mataifa kuwa wangu mwenyewe.

27 " 'Mwanaume au mwanamke ambaye ni mchawi, mwaguzi au mwenye kupunga pepo miongoni mwenu lazima auawe. Mtawapiga kwa

mawe; nayo damu yao itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.’ ”

# 21

*Sheria kwa ajili ya makuhani*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa, “Sema
na makuhani, wana wa Haruni, uwaambie:
‘Kamwe kuhani asijitie unajisi kwa ajili ya mtu
wake yeyote anayekufa,
2 isipokuwa jamaa wake wa karibu, kama vile
mama yake au baba yake, mwanawe au binti
yake, ndugu yake,
3 au dada yake asiyeolewa ambaye anamtege-
mea kwa kuwa hana mume, kwa ajili ya hao
aweza kujitia unajisi.
4 Kamwe asijitie unajisi mwenyewe kutokana
na wale watu ambao anahusiana nao kwa
kuoana, na hivyo kujitia unajisi.
5 “ ‘Kamwe makuhani wasinyoe nywele za
vichwa vyao wala wasinyoe pembeni mwa ndevu
zao, au kuweka chale kwenye miili yao.
6 Lazima wawe watakatifu kwa Mungu wao,
na kamwe wasilinajisi jina la Mungu wao. Kwa
sababu ndio wanaotoa sadaka za kuteketezwa
kwa moto kwa Mwenyezi Mungu, chakula cha
Mungu wao, hivyo lazima wawe watakatifu.
7 “ ‘Kamwe wasioe wanawake waliojinajisi kwa
ukahaba, au waliopewa talaka na waume wao,
kwa sababu makuhani ni watakatifu kwa Mungu
wao.
8 Waoneni kuwa watakatifu, kwa sababu ndio
wanaotoa chakula cha Mungu wenu. Kumbukeni
kuwa ni watakatifu, kwa sababu Mimi Mwenyezi

Mungu ni mtakatifu, Mimi niwafanyaye ninyi kuwa watakatifu.

9 " 'Ikiwa binti ya kuhani anajitia unajisi kwa kufanya ukahaba, anamwaibisha baba yake; lazima achomwe kwa moto.

10 " 'Kuhani mkuu, yule miongoni mwa ndugu zake ambaye amekwisha kupakwa mafuta kwa kumiminiwa juu ya kichwa chake, na ambaye amewekwa wakfu kuvaa mavazi ya ukuhani, kamwe asiache nywele zake bila kufunikwa, wala asirarue nguo zake.
11 Kamwe asiingie mahali palipo maiti ndani. Kamwe asijitie unajisi, hata kwa ajili ya baba yake au mama yake,
12 wala asiondoke mahali patakatifu pa Mungu wake au kupanajisi, kwa sababu amewekwa wakfu kwa mafuta ya Mungu wake. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.

13 " 'Mwanamke atakayeolewa na kuhani lazima awe bikira.
14 Kamwe asimwoe mjane, au mwanamke aliyepewa talaka, wala mwanamke aliyejinajisi kwa ukahaba, bali atamwoa tu bikira kutoka miongoni mwa watu wake,
15 na hivyo hatawatia unajisi wazao wake miongoni mwa watu wake. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, nimfanyaye mtakatifu.' "

16 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
17 "Mwambie Haruni: 'Kwa vizazi vijavyo, hakuna mzao wako mwenye dosari atakayekaribia kutoa chakula cha Mungu wake.

18 Hakuna mtu mwenye dosari yoyote awezaye
kukaribia: hakuna mtu aliye kipofu au kiwete, au
aliyeharibika uso au asiye na viungo kamili,
19 hakuna mtu mwenye mguu au mkono uliole-
maa,
20 au mwenye kibiongo au aliyedumaa, au aliye
na tatizo la macho, au aliye na uvimbe wenye
usaha au majipu, au aliyehasiwa.
21 Hakuna mzao wa kuhani Haruni mwenye
kilema chochote atakayekaribia kutoa sadaka ya
kuteketezwa kwa moto kwa Mwenyezi Mungu.
Kama ana kilema, kamwe asikaribie kutoa
chakula cha Mungu wake.
22 Anaweza kula chakula kitakatifu sana cha
Mungu wake, pia hata chakula kitakatifu.
23 Lakini kwa sababu ya kilema chake, kamwe
asikaribie pazia wala kukaribia madhabahu,
asije akanajisi mahali patakatifu pangu. Mimi
ndimi Mwenyezi Mungu, niwafanyaye watakat-
ifu.' ”
24 Basi Musa akanena na Haruni, na wanawe,
na Waisraeli wote.

# 22

*Matumizi ya sadaka takatifu*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
2 “Mwambie Haruni na wanawe kushughulikia
kwa uangalifu sadaka takatifu Waisraeli wana-
zoziweka wakfu kwangu, ili wasilinajisi Jina
langu takatifu. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.
3 “Waambie: ‘Katika vizazi vijavyo, ikiwa
yeyote wa wazao wako ni najisi, naye akakaribia
sadaka takatifu zile Waisraeli wanazoweka

wakfu kwa Mwenyezi Mungu, mtu huyo lazima akatiliwe mbali na uso wangu. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.

4 " 'Ikiwa mzao wa Haruni ana ugonjwa
wa ngozi unaoambukiza au anatokwa na usaha mwilini, hawezi kula sadaka takatifu hadi atakasike. Pia atakuwa najisi akigusa kitu chochote kilicho najisi kutokana na kugusa maiti, au akigusa mtu aliyetokwa na shahawa,
5 au akigusa kitu chochote kinachotambaa kim-
fanyacho mtu najisi, au mtu yeyote awezaye kumtia unajisi, hata unajisi uwe gani.
6 Mtu anayegusa kitu chochote cha aina hiyo
atakuwa najisi hadi jioni. Kamwe hatakula sadaka yoyote takatifu hadi yeye mwenyewe awe ameoga kwa maji.
7 Jua linapotua, atakuwa safi, na baadaye
anaweza kula sadaka takatifu, kwa kuwa ni vyakula vyake.
8 Kamwe asile nyama ya mzoga wala iliy-
oraruliwa na wanyama pori, naye akatiwa unajisi kwa hilo. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu.

9 " 'Makuhani lazima washike maagizo yangu
ili wasiwe na hatia, wakafa kwa kuyadharau. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu ninayewafanya watakatifu.

10 " 'Hakuna mtu yeyote asiye wa jamaa ya
kuhani anayeruhusiwa kula sadaka takatifu, hata mgeni wa kuhani au mfanyakazi wake haruhusiwi kuila.
11 Lakini ikiwa kuhani amenunua mtumwa
kwa fedha, au mtumwa amezaliwa katika

nyumba ya kuhani huyo, mtumwa huyo aweza kula chakula cha huyo kuhani.

12 Ikiwa binti ya kuhani ameolewa na mtu asiye kuhani, binti huyo haruhusiwi kula chochote cha matoleo matakatifu.

13 Lakini ikiwa binti ya kuhani amekuwa mjane au amepewa talaka, naye hana watoto, na akarudi kuishi na jamaa ya baba yake kama wakati wa usichana wake, binti huyo anaweza kula chakula cha baba yake. Hata hivyo, mtu asiyeruhusiwa hawezi kula chochote katika chakula hiki.

14 " 'Ikiwa mtu yeyote amekula sadaka takatifu kwa makosa, lazima atoe malipo ya sadaka hiyo kwa kuhani na kuongeza sehemu ya tano ya thamani ya sadaka hiyo.

15 Kamwe makuhani wasiinajisi sadaka takatifu ambayo Waisraeli wameitoa kwa Mwenyezi Mungu

16 kwa kuwaruhusu kuzila sadaka hizo takatifu, na hivyo kuwaletea hatia ya kudaiwa malipo. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu niwafanyaye watakatifu.' "

### *Dhabihu zisizokubalika*

17 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,

18 "Sema na Haruni na wanawe, na Waisraeli wote uwaambie: 'Ikiwa mmoja wenu, aliye Mwisraeli au mgeni anayeishi katika nchi ya Israeli, atatoa matoleo kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa kwa moto kwa Mwenyezi Mungu, iwe kutimiza nadhiri au kuwa sadaka ya hiari,

19 lazima amtoe mnyama dume asiye na dosari,
akiwa ng'ombe, mbuzi au kondoo, ili aweze
kukubalika kwa niaba yako.
20 Kamwe usitoe kitu chochote chenye dosari
kwa sababu hakitakubaliwa kwa niaba yako.
21 Mtu yeyote aletapo sadaka ya amani kwa
Mwenyezi Mungu kutoka kundi la ng'ombe au la
mbuzi ili kutimiza nadhiri maalum au sadaka ya
hiari, lazima sadaka hiyo isiwe na dosari au waa
ili ikubalike.
22 Kamwe usimtolee Mwenyezi Mungu
mnyama aliye kipofu, aliyejeruhiwa wala aliye
kilema, au chochote kilicho na uvimbe, au
chenye upele au vidonda vinavyotoka usaha.
Kamwe chochote cha aina hii kisiwekwe juu
ya madhabahu kuwa sadaka iliyotolewa kwa
Mwenyezi Mungu ya kuteketezwa kwa moto.
23 Lakini unaweza ukamtoa ng'ombe au kon-
doo mwenye kilema au aliyedumaa kuwa sadaka
ya hiari, lakini hii haitakubalika kuwa sadaka ya
kutimiza nadhiri.
24 Kamwe usimtolee Mwenyezi Mungu
mnyama ambaye mapumbu yake yamejeruhiwa,
au kuhasiwa, au kuraruliwa au kukatwa. Kamwe
usifanye hivi katika nchi yako mwenyewe,
25 na kamwe usikubali wanyama wa aina hii
kutoka mkono wa mgeni ili kuwatoa wanyama
hao kuwa chakula kwa Mungu wako. Wanyama
hao hawatakubaliwa kwa niaba yako, kwa
sababu wana vilema, nao wana dosari.' "
26 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
27 "Ndama, mwana-kondoo au mwana-mbuzi
anapozaliwa, atabaki na mama yake kwa siku

saba. Kuanzia siku ya nane na kuendelea
anaweza kukubaliwa kuwa sadaka iliyotolewa
kwa Mwenyezi Mungu kwa kuteketezwa kwa
moto.
28 Usimchinje ng'ombe na ndama wake, au
kondoo na kitoto chake siku moja.

29 "Unapomtolea Mwenyezi Mungu dhabihu ya
shukrani, itoe kwa namna ambayo itakubalika
kwa niaba yako.
30 Ni lazima iliwe siku hiyo hiyo, pasipo
kubakiza chochote hadi asubuhi. Mimi ndimi
Mwenyezi Mungu.

31 "Shikeni maagizo yangu na kuyafuata. Mimi
ndimi Mwenyezi Mungu.
32 Msilinajisi Jina langu takatifu. Lazima
nikubalike kuwa mtakatifu kwa Waisraeli.
Mimi ndimi Mwenyezi Mungu ninayewafanya
watakatifu,
33 na niliyewatoa katika nchi ya Misri niwe
Mungu wenu. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu."

# 23

### *Sikukuu zilizoamriwa*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
2 "Sema na Waisraeli na uwaambie: 'Hizi ndizo
sikukuu zangu zilizoamriwa, sikukuu zilizoam-
riwa za Mwenyezi Mungu, ambazo mtazitangaza
kuwa makusanyiko matakatifu.

### *Sabato*

3 " 'Kuna siku sita mnazoweza kufanya kazi,
lakini siku ya saba ni Sabato ya kupumzika, siku

ya kusanyiko takatifu. Hamtafanya kazi yoyote. Popote mnapoishi, ni Sabato kwa Mwenyezi Mungu.

### *Pasaka na Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu (Hesabu 28:16-25)*

4 " 'Hizi ni sikukuu za Mwenyezi Mungu zilizoamriwa, makusanyiko matakatifu mtakayoyatangaza kwa nyakati zilizoamriwa:
5 Pasaka ya Mwenyezi Mungu huanza jioni ya siku ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza.
6 Siku ya kumi na tano ya mwezi huo wa kwanza, Sikukuu ya Mwenyezi Mungu ya Mikate Isiyotiwa Chachu huanza; kwa siku saba, mtakula mikate isiyotiwa chachu.
7 Katika siku ya kwanza, mtakuwa na kusanyiko takatifu, na msifanye kazi zenu za kawaida.
8 Kwa siku saba mtamletea Mwenyezi Mungu sadaka ya kuteketezwa kwa moto. Kwenye siku hiyo ya saba mtafanya kusanyiko takatifu, na msifanye kazi zenu za kawaida.' "

### *Malimbuko*

9 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
10 "Sema na Waisraeli na uwaambie: 'Mtakapoingia katika nchi nitakayowapa na kuvuna mazao ya nchi hiyo, leteni kwa kuhani mganda wa nafaka ya kwanza mtakayovuna.
11 Naye atauinua huo mganda mbele za Mwenyezi Mungu ili ukubaliwe kwa niaba yenu; kuhani ataupunga siku inayofuata Sabato.
12 Siku hiyo mtakapoinua huo mganda, lazima mtoe kwa Mwenyezi Mungu dhabihu ya

kuteketezwa kwa moto ya mwana-kondoo wa
mwaka mmoja asiye na dosari,
13 pamoja na sadaka yake ya nafaka ya se-
hemu mbili za kumi ya efa* ya unga laini
uliochanganywa na mafuta, sadaka iliyotolewa
kwa Mwenyezi Mungu kwa kuteketezwa kwa
moto; hii itakuwa sadaka iliyo harufu nzuri ya
kupendeza, na sadaka yake ya kinywaji ya robo
ya hini† ya divai.
14 Kamwe msile mkate wowote, au nafaka
iliyokaangwa au nafaka mpya, hadi siku ile
mtakayomletea Mungu wenu sadaka hii. Hili
litakuwa agizo la kudumu kwa vizazi vijavyo,
popote mnapoishi.

### *Sikukuu ya Majuma (Hesabu 28:26-31)*

15 " 'Tangu siku ile iliyofuata Sabato, siku mliy-
otoa sadaka ya mganda wa kuinuliwa, hesabuni
majuma saba kamili.
16 Mtahesabu siku hamsini hadi siku inayofu-
ata Sabato ya saba, ndipo mtatoa sadaka ya
nafaka mpya kwa Mwenyezi Mungu.
17 Kutoka popote mnapoishi, mtaleta mikate
miwili iliyotengenezwa kwa sehemu mbili za
kumi ya efa moja ya unga laini, uliookwa kwa
chachu, kuwa sadaka ya kuinuliwa ya malim-
buko kwa Mwenyezi Mungu.
18 Toeni pamoja na hiyo mikate wana-kondoo
saba, kila mmoja wa mwaka mmoja asiye na
dosari, na fahali mchanga, na kondoo dume

* **23:13** Sehemu mbili za kumi ya efa ni sawa na kilo mbili.
† **23:13** Robo ya hini ni sawa na lita moja.

wawili. Watakuwa sadaka ya kuteketezwa kwa
moto iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu, pamoja
na sadaka za nafaka na sadaka za vinywaji,
sadaka iliyotolewa kwa moto yenye harufu nzuri
ya kumpendeza Mwenyezi Mungu.
19 Kisha toeni dhabihu ya beberu mmoja kwa
ajili ya sadaka ya dhambi, na wana-kondoo waw-
ili, kila mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili ya
sadaka ya amani.
20 Kuhani atawainua hao wana-kondoo wawili
mbele za Mwenyezi Mungu kuwa sadaka ya
kuinuliwa, pamoja na mkate wa malimbuko. Ni
sadaka takatifu kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili
ya kuhani.
21 Siku hiyo hiyo mtatangaza kusanyiko takat-
ifu, na msifanye kazi zenu za kawaida. Hili
litakuwa agizo la kudumu kwa vizazi vijavyo,
popote mtakapoishi.

22 " 'Mnapovuna mavuno ya ardhi yenu,
msivune hadi mpakani mwa shamba lenu, au
kukusanya masazo ya mavuno yenu. Hayo
utayaacha kwa ajili ya maskini na mgeni. Mimi
ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu.' "

### *Sikukuu ya Tarumbeta (Hesabu 29:1-6)*

23 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
24 "Waambie Waisraeli: 'Katika siku ya kwanza
ya mwezi wa saba mtakuwa na Sabato ya
mapumziko, kusanyiko takatifu la ukumbusho
litakaloadhimishwa kwa kupiga tarumbeta.

25 Msifanye kazi zenu zozote za kawaida,
lakini toeni sadaka kwa Mwenyezi Mungu iliy-
oteketezwa kwa moto.' "

### *Siku ya Upatanisho (Hesabu 29:7-11)*

26 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
27 "Siku ya kumi ya mwezi huu wa saba ni Siku
ya Upatanisho. Mtafanya kusanyiko takatifu,
mfunge, na kutoa sadaka ya kuteketezwa kwa
moto kwa Mwenyezi Mungu.
28 Msifanye kazi siku hiyo, kwa sababu ni Siku
ya Upatanisho, ambapo upatanisho unafanyika
kwa ajili yenu mbele za Mwenyezi Mungu,
Mungu wenu.
29 Mtu ambaye hatafunga siku hiyo ni lazima
akatiliwe mbali na watu wake.
30 Mtu atakayefanya kazi siku hiyo nita-
mwangamiza kutoka miongoni mwa watu wake.
31 Hamtafanya kazi kamwe. Hili litakuwa agizo
la kudumu kwa vizazi vijavyo popote mnapoishi.
32 Ni Sabato ya mapumziko kwenu, na lazima
mfunge. Tangu jioni ya siku ya tisa ya mwezi hadi
jioni inayofuata, mtaishika Sabato yenu."

### *Sikukuu ya Vibanda (Hesabu 29:12-40)*

33 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
34 "Waambie Waisraeli: 'Katika siku ya kumi
na tano ya mwezi wa saba, Sikukuu ya vibanda
itaanza, nayo itaadhimishwa kwa siku saba kwa
Mwenyezi Mungu.
35 Siku ya kwanza ni kusanyiko takatifu, msi-
fanye kazi zenu za kawaida.

36 Kwa siku saba toeni sadaka kwa Mwenyezi
Mungu za kuteketezwa kwa moto. Kwenye siku
ya nane fanyeni kusanyiko takatifu, na kutoa
sadaka ya kuteketezwa kwa moto kwa Mwenyezi
Mungu. Ni kusanyiko la mwisho, msifanye kazi
zenu za kawaida.

37 (“ ‘Hizi ni sikukuu za Mwenyezi Mungu zili-
zoamriwa, ambazo mtazitangaza kuwa maku-
sanyiko matakatifu kwa kuleta sadaka kwa
Mwenyezi Mungu za kuteketeza kwa moto:
sadaka za kuteketezwa na sadaka za nafaka,
dhabihu na sadaka za vinywaji zitahitajika kila
siku.
38 Sadaka hizi ni nyongeza ya zile mnazozitoa
katika Sabato za Mwenyezi Mungu, na pia ni ny-
ongeza ya matoleo yenu ya chochote mlichoweka
nadhiri, na sadaka zenu zote za hiari mnazozitoa
kwa Mwenyezi Mungu.)

39 “ ‘Basi kuanzia siku ya kumi na tano ya
mwezi wa saba, baada ya kuvuna mazao yote
ya nchi, mtaadhimisha sikukuu kwa Mwenyezi
Mungu kwa siku saba; siku ya kwanza ni Sabato
ya mapumziko, na pia siku ya nane ni Sabato ya
mapumziko.
40 Siku ya kwanza mtachukua matunda mazuri
ya miti, matawi ya mitende, matawi yenye
majani mengi, na matawi ya mirebi, nanyi
mtashangilia mbele za Mwenyezi Mungu, Mungu
wenu, kwa siku saba.
41 Mtaadhimisha siku hii kuwa sikukuu kwa
Mwenyezi Mungu kwa siku saba kila mwaka. Hili
litakuwa agizo la kudumu kwa vizazi vijavyo;
iadhimisheni mwezi wa saba.

42 Mtaishi katika vibanda kwa siku saba:
Wazawa wote wa Waisraeli wataishi katika
vibanda,
43 ili wazao wenu wajue kuwa niliwafanya
Waisraeli waishi kwenye vibanda nilipowatoa
Misri. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu
wenu.' "
44 Kwa hiyo Musa akawatangazia Waisraeli
sikukuu zilizoamriwa na Mwenyezi Mungu.

# 24

## *Mafuta na mikate mbele za Mwenyezi Mungu*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,
2 "Waagize Waisraeli wakuletee mafuta safi ya
zeituni yaliyokamuliwa kwa ajili ya mwanga ili
taa ziwe zinawaka daima.
3 Nje ya pazia la Sanduku la Ushuhuda ndani
ya Hema la Kukutania, Haruni ataziwasha taa
mbele za Mwenyezi Mungu kuanzia jioni hadi
asubuhi daima. Hili litakuwa agizo la kudumu
kwa vizazi vijavyo.
4 Taa zilizo juu ya kinara cha dhahabu safi
mbele za Mwenyezi Mungu lazima zihudumiwe
daima.
5 "Chukua unga laini, uoke mikate kumi na
miwili, ukitumia sehemu mbili za kumi ya efa*
ya unga kwa kila mkate.
6 Iweke katika mistari miwili, kila mstari
mikate sita, uiweke mbele za Mwenyezi Mungu
juu ya meza iliyotengenezwa kwa dhahabu safi.

---

* **24:5** Sehemu mbili za kumi ya efa ni sawa na kilo mbili.

7 Kando ya kila mstari, weka uvumba safi kama
sehemu ya kumbukumbu ili kuwakilisha mikate
kuwa sadaka iliyotolewa kwa Mwenyezi Mungu
kwa kuteketezwa kwa moto.
8 Mikate hii itawekwa mbele za Mwenyezi
Mungu kila wakati, Sabato baada ya Sabato, kwa
niaba ya Waisraeli, kuwa agano la kudumu.
9 Hii ni mali ya Haruni na wanawe, watakaoila
katika mahali patakatifu, kwa sababu ni sehemu
takatifu sana ya fungu lao milele la sadaka iliy-
otolewa kwa Mwenyezi Mungu kwa kuteketezwa
kwa moto."

### *Mwenye kukufuru apigwa mawe*

10 Basi mwana wa mama Mwisraeli na baba
Mmisri alienda miongoni mwa Waisraeli, nayo
mapigano yakatokea ndani ya kambi kati yake na
Mwisraeli.
11 Huyu mwana wa mwanamke Mwisraeli aka-
likufuru Jina la Mwenyezi Mungu kwa kulaani;
kwa hiyo wakamleta kwa Musa. (Mama yake
aliitwa Shelomithi binti Dibri, wa kabila la Dani.)
12 Nao wakamweka mahabusu hadi mapenzi
ya Mwenyezi Mungu yawe wazi kwao.

13 Ndipo Mwenyezi Mungu akamwambia
Musa:
14 "Mchukue huyo aliyekufuru nje ya kambi.
Wale wote waliomsikia akikufuru wataweka
mikono juu ya kichwa chake, kisha kusanyiko
lote watampiga mawe.
15 Waambie Waisraeli: 'Ikiwa mtu yeyote atam-
laani Mungu wake, atakuwa na hatia kwa uovu
wake.

16 Yeyote atakayekufuru Jina la Mwenyezi
Mungu ni lazima auawe. Kusanyiko lote
watampiga kwa mawe. Iwe ni mgeni au mzawa,
atakapolikufuru Jina la Mwenyezi Mungu, ni
lazima auawe.
17 " 'Kama mtu yeyote atamuua mtu mwingine,
ni lazima auawe.
18 Mtu yeyote auaye mnyama wa mtu
mwingine lazima afidie, uhai kwa uhai.
19 Ikiwa mtu yeyote atamjeruhi jirani yake,
chochote alichomtenda naye atatendewa:
20 iwapo amemvunja mfupa atavunjwa
mfupa, jicho kwa jicho, jino kwa jino. Kama
alivyomjeruhi mwenzake, vivyo hivyo ndivyo
atakavyojeruhiwa.
21 Yeyote auaye mnyama wa mtu lazima alipe
fidia, lakini yeyote auaye mtu, lazima auawe.
22 Mtakuwa na sheria hiyo hiyo kwa mgeni
na kwa mzawa. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu,
Mungu wenu.' "

23 Kisha Musa akasema na Waisraeli, nao
wakamchukua yule aliyekufuru nje ya kambi
na kumpiga mawe. Waisraeli wakafanya kama
Mwenyezi Mungu alivyomwagiza Musa.

# 25

### *Mwaka wa Sabato*
### *(Kumbukumbu 15:1-11)*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa katika
Mlima Sinai,
2 "Sema na Waisraeli uwaambie: 'Mtakapoingia
katika nchi ninayowapa ninyi, nchi yenyewe

ni lazima ishike sabato kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

3 Kwa miaka sita mtapanda mazao katika mashamba yenu, nanyi kwa miaka sita mtaikata mizabibu yenu matawi na kuvuna mazao yake.

4 Lakini katika mwaka wa saba, nchi lazima iwe na sabato ya mapumziko, sabato kwa Mwenyezi Mungu. Msipande mbegu katika mashamba yenu, wala msikate mizabibu yenu matawi.

5 Msivune chochote kinachoota chenyewe, wala kuvuna zabibu zenu ambazo hamkuzihudumia. Nchi lazima iwe na mwaka wa mapumziko.

6 Chochote nchi itoacho katika mwaka wa sabato kitakuwa chakula chenu wenyewe, watumishi wenu wa kiume na wa kike, mfanyakazi aliyeajiriwa, na mkazi wa muda anayeishi miongoni mwenu,

7 vilevile malisho ya mifugo yenu na wanyama pori katika nchi yenu. Chochote nchi itakachozalisha kinaweza kuliwa.

### *Mwaka wa Yubile*

8 " 'Hesabu sabato saba za miaka saba, yaani miaka saba mara saba, ili sabato saba za miaka saba ziwe muda wa miaka arobaini na tisa.

9 Ndipo tarumbeta itapigwa kila mahali katika siku ya kumi ya mwezi wa saba. Katika Siku ya Upatanisho, piga tarumbeta katika nchi yako yote.

10 Mwaka wa hamsini mtauweka wakfu na kutangaza uhuru katika nchi kwa wakazi wake

wote. Itakuwa ni Yubile* kwenu; kila mmoja
wenu atairudia mali ya jamaa yake, na kila
mmoja kurudi kwenye ukoo wake.
11 Mwaka wa hamsini utakuwa Yubile
kwenu, msipande wala msivune kile kinachoota
chenyewe, au kuvuna zabibu zisizohudumiwa.
12 Kwa kuwa ni Yubile, nayo itakuwa takatifu
kwenu; mtakula tu kile kilichotoka moja kwa
moja mashambani.
13 " 'Katika huu Mwaka wa Yubile, kila mmoja
atarudi kwenye mali yake mwenyewe.
14 " 'Ikiwa utauza ardhi kwa mmoja wa wazawa
wa nchi yako, au ukinunua ardhi kutoka kwake,
mmoja asimpunje mwingine.
15 Utanunua ardhi kwa mzawa wa nchi yako
kulingana na hesabu ya miaka baada ya Yu-
bile. Naye muuzaji ataiuza kwako kulingana na
hesabu ya miaka iliyobaki ya kuvuna mavuno.
16 Miaka inapokuwa mingi, utaongeza bei,
nayo miaka ikiwa michache, utapunguza bei,
kwa sababu kile anachokuuzia kwa hakika ni
hesabu ya mazao.
17 Mmoja asimpunje mwingine, bali utamcha
Mungu wako. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu,
Mungu wako.
18 " 'Fuateni amri zangu na mwe waangalifu
kutii amri zangu, nanyi mtaishi salama katika
nchi.
19 Kisha nchi itazaa matunda yake, nanyi
mtakula na kushiba na kuishi humo kwa salama.

* **25:10** Yubile ni baragumu iliyopigwa kila mwaka wa hamsini; ni Sabato ya nchi ya kila mwaka wa hamsini uliokuwa mwaka wa ukombozi, yaani kuachia huru.

20 Mwaweza kuuliza, “Tutakula nini katika
mwaka wa saba ikiwa hatutapanda wala kuvuna
mazao yetu?”
21 Nitawaletea baraka ya pekee katika mwaka
wa sita, ili nchi iweze kuzalisha mazao ya
kuwatosha kwa miaka mitatu.
22 Mnapopanda mwaka wa nane, mtakula
mavuno ya miaka iliyopita, na mtaendelea
kuyala mazao hayo hadi mvune mavuno ya
mwaka wa tisa.

23 “ ‘Kamwe ardhi isiuzwe kwa mkataba wa
kudumu, kwa sababu nchi ni mali yangu, nanyi
ni wageni na wapangaji wangu.
24 Katika nchi yote mtakayoshika kuwa milki
yenu, ni lazima mtoe ukombozi wa ardhi.

25 “ ‘Ikiwa mmoja wa wazawa wa nchi yako
amekuwa maskini na akauza baadhi ya mali
yake, ndugu yake wa karibu atakuja na kukom-
boa kile ndugu yake alichokiuza.
26 Iwapo mtu huyo hana jamaa wa karibu wa
kukomboa mali hiyo kwa ajili yake, lakini yeye
mwenyewe akafanikiwa na kupata mali itoshayo
kuikomboa,
27 ataamua tena thamani yake kwa miaka
tangu alipoiuza, na kurudisha kiasi kilichobaki
cha thamani kwa mtu aliyekuwa amemuuzia
mali hiyo, naye ataweza kuirudia mali yake.
28 Lakini kama hatapata njia ya kumlipa
mnunuzi, ile mali aliyouza itabaki kumilikiwa
na mnunuzi hadi Mwaka wa Yubile. Mali hiyo
itarudishwa Mwaka wa Yubile, naye ataweza
kuirudia mali yake.

29 “ ‘Ikiwa mtu atauza nyumba iliyo ndani ya
mji uliozungukwa kwa ukuta, yeye anayo haki
ya kuikomboa mwaka mzima baada ya mauzo ya
hiyo nyumba. Wakati huo anaweza kuikomboa.
30 Ikiwa haikukombolewa kabla ya mwaka
mmoja kamili kupita, nyumba iliyo ndani ya
mji uliozungukwa kwa ukuta itakuwa mali ya
kudumu ya mnunuzi na wazao wake. Haitarud-
ishwa Mwaka wa Yubile.
31 Lakini nyumba zilizo vijijini bila ya kuwa
na kuta zilizozizunguka zitahesabiwa kama
mashamba. Zinaweza kukombolewa, nazo zirud-
ishwe Mwaka wa Yubile.

32 “ ‘Walawi siku zote wana haki ya kukomboa
nyumba zao katika miji ya Walawi wanayoimi-
liki.
33 Kwa hiyo mali ya Mlawi inaweza kukom-
bolewa, yaani nyumba iliyouzwa katika mji
wowote wanaoushikilia itarudishwa Mwaka wa
Yubile, kwa sababu nyumba zilizo katika miji ya
Walawi ni mali yao miongoni mwa Waisraeli.
34 Lakini maeneo ya malisho yaliyo mali ya miji
yao kamwe yasiuzwe, ni milki yao ya kudumu.

35 “ ‘Ikiwa mmoja wa wazawa wa nchi yako
amekuwa maskini, naye akashindwa kujitege-
meza mwenyewe kati yako, msaidie vile ungem-
saidia mgeni au mkazi wa muda, ili aweze kuen-
delea kuishi kati yako.
36 Usichukue riba wala faida yoyote kutoka
kwake, bali utamwogopa Mungu wako, ili mzawa
wa nchi yako aweze kuendelea kuishi kati yako.
37 Usimkopeshe fedha ili alipe na riba, wala
usimuuzie chakula kwa faida.

38 Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wako,
niliyekuleta kutoka nchi ya Misri nikupe nchi ya
Kanaani, nami niwe Mungu wako.

39 “ ‘Ikiwa mmoja wa wazawa wa nchi yako
amekuwa maskini kati yako, naye akajiuza
kwako, usimfanye atumike kama mtumwa.
40 Atatendewa kama mfanyakazi aliyeajiriwa,
au kama mkazi wa muda katikati yako; naye
atatumika hadi Mwaka wa Yubile.
41 Ndipo yeye na watoto wake wataachiwa,
naye atarudi kwa watu wa ukoo wake, na kwenye
mali ya baba zake.
42 Kwa sababu Waisraeli ni watumishi wangu
niliowaleta kutoka nchi ya Misri, kamwe wasi-
uzwe kama watumwa.
43 Usiwatawale kwa ukatili, lakini utamcha
Mungu wako.

44 “ ‘Watumwa wako wa kiume na wa kike wata-
toka katika mataifa yanayokuzunguka; unaweza
kununua watumwa kutoka kwao.
45 Pia unaweza kununua baadhi ya wakazi wa
muda wanaoishi kati yako, na jamaa ya koo zao
waliozaliwa katika nchi yako; nao watakuwa
mali yako.
46 Unaweza kuwafanya hao kuwa urithi wa
watoto wako, na unaweza kuwafanya watumwa
kwa maisha yao yote. Lakini usiwatawale ndugu
zako Waisraeli kwa ukatili.
47 “ ‘Ikiwa mgeni au mkazi wa muda katikati
yako atakuwa tajiri, na mmoja wa wazawa wa
nchi yako akawa maskini, naye akajiuza kwa
yule mgeni anayeishi katikati yako, au kwa
mmoja wa jamaa wa koo za wageni,

48 anayo haki ya kukombolewa baada ya kuji-
uza. Mmoja wa jamaa zake aweza kumkomboa:
49 Mjomba wake, au binamu yake, au yeyote
aliye ndugu wa damu katika ukoo wake aweza
kumkomboa. Au akifanikiwa, anaweza kujikom-
boa mwenyewe.
50 Yeye na huyo aliyemnunua watahesabu
muda kuanzia mwaka aliojiuza hadi Mwaka wa
Yubile. Bei ya kuachiwa kwake itakadiriwa
kulingana na ujira unaolipwa mfanyakazi wa
kuajiriwa kwa idadi ya hiyo miaka.
51 Ikiwa imebaki miaka mingi, ni lazima atal-
ipia ukombozi wake fungu kubwa la bei iliy-
olipwa kumnunua.
52 Ikiwa miaka iliyobaki ni michache kufikia
Mwaka wa Yubile, atafanya hesabu yake, naye
atalipa malipo yanayostahili kwa ajili ya ukom-
bozi wake.
53 Atatendewa kama mtu wa kuajiriwa mwaka
hadi mwaka; lazima uone kwamba yule aliyem-
nunua hamtawali kwa ukatili.
54 “ ‘Hata ikiwa hakukombolewa kwa njia mo-
jawapo ya hizi, yeye na watoto wake wataachiwa
katika Mwaka wa Yubile,
55 kwa kuwa kwangu, Waisraeli ni watumishi.
Ni watumishi wangu niliowatoa kutoka nchi ya
Misri. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu
wako.

# 26

*Thawabu ya utii*
*(Kumbukumbu 7:12-24; 28:1-14)*

1 “ ‘Msijitengenezee sanamu, au kusimamisha
sanamu ya kuchonga, au jiwe la kuabudia, na pia
msijiwekee jiwe lililochongwa katika nchi yenu
ili kulisujudia. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu,
Mungu wenu.
2 “ ‘Zishikeni Sabato zangu na kuheshimu ma-
hali patakatifu pangu. Mimi ndimi Mwenyezi
Mungu.
3 “ ‘Ikiwa mtafuata amri zangu na kuwa waan-
galifu kutii maagizo yangu,
4 nitawanyeshea mvua katika majira yake,
nayo ardhi itatoa mazao yake, na miti ya
mashambani itazaa matunda yake.
5 Kupura nafaka kwenu kutaendelea hadi
wakati wa kuvuna zabibu. Na kuvuna zabibu
kutaendelea hadi wakati wa kupanda mbegu,
nanyi mtakula na kushiba, na mtaishi salama
katika nchi yenu.
6 “ ‘Nitawapa amani katika nchi, mpate kulala
pasipo kutiwa hofu na yeyote. Nitawaondoa
wanyama wakali watoke kwenye nchi, nao up-
anga hautapita katika nchi yenu.
7 Mtawafukuza adui zenu, nanyi mtawaua kwa
upanga mbele yenu.
8 Watu wenu watano watafukuza adui mia
moja, na watu wenu mia moja watafukuza adui
elfu kumi, nao adui zenu wataanguka kwa up-
anga mbele yenu.
9 “ ‘Nitawaangalia kwa upendeleo na
kuwafanya mzae na kuzidisha idadi yenu, nami
nitalishika agano langu na ninyi.
10 Wakati wa kuvuna mtakuwa bado mnakula
mavuno ya mwaka uliopita, na itawalazimu

kuyaondoa ghalani ili mpate nafasi ya mavuno mapya.
11 Nitafanya makao yangu miongoni mwenu, nami sitawachukia.
12 Nitatembea kati yenu niwe Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wangu.
13 Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu,
niliyewatoa katika nchi ya Misri ili msiendelee kuwa watumwa wa Wamisri, nikavunja nira yenu, na kuwawezesha kutembea mkiwa mmeinua vichwa vyenu.

### *Adhabu ya kutokutii (Kumbukumbu 28:15-68)*

14 “ ‘Lakini kama hamtanisikiliza na kutimiza maagizo haya yote,
15 nanyi kama mtazikataa amri zangu na kuzichukia sheria zangu, tena mkishindwa kutimiza amri zangu zote, na hivyo mkavunja agano langu,
16 ndipo nitakapowafanyia hili: Nitawaletea juu yenu hofu ya ghafula, magonjwa ya kudhoofisha, na homa itakayopofusha macho yenu na kuwaondolea uhai wenu. Mtapanda mbegu bila mafanikio, kwa sababu adui zenu watazila.
17 Nitauelekeza uso wangu dhidi yenu ili mshindwe na adui zenu; wale wanaowachukia watawatawala, nanyi mtakimbia ingawa hakuna mtu anayewafukuza.

18 “ ‘Kama baada ya haya yote hamtanisikiliza, nitawaadhibu mara saba zaidi kwa ajili ya dhambi zenu.

19 Nitakivunja kiburi chenu cha ukaidi, na
kuifanya anga iliyo juu yenu iwe kama chuma,
na ardhi yenu kama shaba.
20 Nguvu zenu zitatumika bila ya mafanikio,
kwa sababu ardhi yenu haitawazalia mazao
yake, wala miti ya nchi yenu haitazaa matunda
yake.

21 " 'Kama mtaendelea kuwa na uadui nami,
na kukataa kunisikiliza, nitawazidishia mateso
yenu mara saba zaidi, kama dhambi zenu zi-
navyostahili.
22 Nitawatuma wanyama mwitu dhidi
yenu, nao watawaibieni watoto wenu,
watawaangamiza ng'ombe wenu, na kuifanya
idadi yenu kuwa ndogo, hivi kwamba barabara
zenu zitakuwa hazina watu.

23 " 'Ikiwa pamoja na mambo haya hamtakubali
maonyo yangu lakini mkaendelea kuweka uadui
nami,
24 mimi mwenyewe nitaweka uadui nanyi, na
kuwatesa kwa ajili ya dhambi zenu mara saba
zaidi.
25 Nitawaletea upanga juu yenu ili kuwap-
atiliza kwa kuvunja agano langu. Mtakapokim-
bilia mijini mwenu, nitatuma tauni kati yenu,
nanyi mtatiwa mikononi mwa adui zenu.
26 Nitakapowaondolea upatikanaji wa mkate
wenu, wanawake kumi wataoka mkate wenu
katika tanuru moja, nao wataugawa mkate ki-
dogo kwa kupima. Mtakula, lakini hamtashiba.

27 " 'Kama hata baada ya haya bado hamtanisik-
iliza lakini mkaendelea kuweka uadui nami,

28 ndipo katika hasira yangu nitaweka uadui nanyi, nami mwenyewe nitawaadhibu mara saba kwa ajili ya dhambi zenu.
29 Mtakula nyama ya wana wenu na nyama ya binti zenu.
30 Nitaharibu mahali penu pa juu pa kuabudia, nibomoe madhabahu yenu ya kufukizia uvumba, na kuzilundika maiti zenu juu ya sanamu zenu zisizo na uhai, nami nitawachukia ninyi.
31 Nitaifanya miji yenu kuwa magofu, na kuharibu mahali patakatifu penu pa kuabudia, nami sitapendezwa na harufu nzuri ya sadaka zenu.
32 Nitaiharibu nchi, ili adui zenu watakaoishi humo washangae.
33 Nitawatawanya ninyi miongoni mwa mataifa, na kuufuta upanga wangu na kuwafuatia. Nchi yenu itaharibiwa, nayo miji yenu itakuwa magofu.
34 Ndipo nchi itafurahia sabato zake muda wote ule itakapokuwa ukiwa, nanyi mkiwa katika nchi ya adui zenu. Ndipo nchi itapumzika na kufurahia sabato zake.
35 Wakati wote nchi itakapobaki ukiwa, itapumzika na kufurahia sabato zake ambazo haikuzipata mlipokuwa mnaishi humo.

36 “ ‘Kwa habari ya wenzenu wale watakaobaki, nitaifanya mioyo yao kuwa na hofu kuu katika nchi za adui zao, kiasi kwamba sauti ya jani linalopeperushwa na upepo itawafanya wakimbie. Watakimbia kana kwamba wanakimbia upanga, nao wataanguka, ijapokuwa hakuna anayewafukuza.

37 Watajikwaa mmoja juu ya mwingine kama
watu wakimbiao upanga, hata ingawa hakuna
anayewafuatia. Hivyo hamtaweza kusimama
mbele ya adui zenu.
38 Mtaangamia kati ya mataifa; nchi ya adui
zenu itawala.
39 Wenzenu watakaobaki wataangamia katika
nchi za adui zao kwa sababu ya dhambi
zao; pia kwa sababu ya dhambi za baba zao
wataangamia.

40 " 'Lakini kama watatubu dhambi zao na
dhambi za baba zao, udanganyifu wao dhidi
yangu na uadui wao kwangu,
41 ambao ulinifanya niwe na uadui nao hata
nikawapeleka katika nchi ya adui zao, wakati
mioyo yao isiyotahiriwa itanyenyekea na kutubu
dhambi yao,
42 nami nitakumbuka agano langu na Yakobo,
na agano langu na Isaka, na agano langu na
Ibrahimu, nami nitaikumbuka nchi.
43 Kwa kuwa wataiacha nchi ukiwa, nayo ita-
furahia sabato zake wakati itakuwa ukiwa bila
wao. Wataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao, kwa
sababu walizikataa sheria zangu na kuzichukia
amri zangu.
44 Lakini pamoja na hili, wakati watakuwa
katika nchi ya adui zao, sitawakataa wala
kuwachukia kiasi cha kuwaangamiza na kuvunja
agano langu nao. Mimi ndimi Mwenyezi Mungu,
Mungu wao.
45 Lakini kwa ajili yao nitalikumbuka agano
langu na baba zao, ambao niliwatoa Misri mbele
ya mataifa ili niwe Mungu wao. Mimi ndimi

Mwenyezi Mungu.’ ”

46 Hizi ndizo amri, sheria na pia masharti
ambazo Mwenyezi Mungu alifanya kati yake
mwenyewe na Waisraeli katika Mlima Sinai kupi-
tia kwa Musa.

# 27

## *Kukomboa kile kilicho cha Mwenyezi Mungu*

1 Mwenyezi Mungu akamwambia Musa,

2 “Sema na Waisraeli uwaambie: ‘Kama mtu
yeyote ataweka nadhiri maalum ili kuweka watu
wakfu kwa Mwenyezi Mungu, kwa kutoa kiasi
cha thamani inayolingana,

3 thamani ya kukomboa mwanaume mwenye
kati ya umri wa miaka ishirini na miaka sitini
itakuwa shekeli hamsini* za fedha, kulingana na
shekeli ya mahali patakatifu;

4 ikiwa ni mwanamke, weka thamani yake kwa
shekeli thelathini†.

5 Kama ni mtu mwenye umri wa miaka kati ya
mitano na ishirini, weka thamani ya mwanaume
kuwa shekeli ishirini‡, na mwanamke shekeli
kumi§.

6 Kama ni mtu mwenye umri kati ya mwezi
mmoja na miaka mitano, weka thamani ya
mwanaume kuwa shekeli tano za fedha, na ile ya
mwanamke kuwa shekeli tatu* za fedha.

---

* **27:3** Shekeli 50 za fedha ni sawa na gramu 600. † **27:4** Shekeli 30 za fedha ni sawa na gramu 360. ‡ **27:5** Shekeli 20 za fedha ni sawa na gramu 240. § **27:5** Shekeli 10 za fedha ni sawa na gramu 120. * **27:6** Shekeli tatu za fedha ni sawa na gramu 36.

7 Kama ni mtu mwenye miaka sitini na zaidi,
weka thamani ya mwanaume kuwa shekeli kumi
na tano†, na mwanamke shekeli kumi.
8 Kama mtu yeyote anayeweka nadhiri ni
maskini mno kuweza kulipa kiasi kilichowekwa,
atampeleka huyo mtu kwa kuhani, ambaye
ataweka thamani yake kulingana na kile yule
anayeweka nadhiri anaweza kulipa.

9 “ ‘Kama kile mtu alichokiwekea nadhiri
ni mnyama anayekubalika kama sadaka kwa
Mwenyezi Mungu, mnyama huyo aliyetolewa
kwa Mwenyezi Mungu anakuwa mtakatifu.
10 Mtu haruhusiwi kumbadilisha au kutoa
mnyama mzuri kwa mbaya, au mnyama mbaya
kwa mzuri. Kama atatoa mnyama badala ya
mwingine, wanyama wote wawili, yaani yule
aliyetolewa na yule aliyebadiliwa, ni watakatifu.
11 Kama alichokiwekea nadhiri ni mnyama
aliye najisi, yaani yule asiyekubalika kuwa
sadaka kwa Mwenyezi Mungu, huyo mnyama
lazima aletwe kwa kuhani,
12 ambaye ataamua ubora wa mnyama
huyo, kama ni mzuri au mbaya. Thamani
yoyote atakayoweka kuhani, hivyo ndivyo
itakavyokuwa.
13 Kama mwenye mnyama atapenda kumkom-
boa mnyama huyo, lazima aongeze sehemu ya
tano ya thamani yake.

14 “ ‘Kama mtu ataweka nyumba yake wakfu
kama kitu kitakatifu kwa Mwenyezi Mungu,
kuhani ataamua ubora wa nyumba hiyo, kama

† **27:7** Shekeli 15 za fedha ni sawa na gramu 180.

ni nzuri au mbaya. Thamani yoyote kuhani atakayoweka, basi hivyo ndivyo itakavyokuwa.
15 Kama mtu aliyeweka nyumba yake wakfu ataikomboa, lazima aongeze sehemu ya tano ya thamani yake, nayo nyumba itakuwa yake tena.
16 " 'Ikiwa mtu ataweka sehemu ya ardhi ya jamaa yake wakfu kwa Mwenyezi Mungu, thamani yake itawekwa kulingana na kiasi cha mbegu inayohitajiwa kupandwa katika ardhi hiyo, yaani homeri‡ moja ya mbegu za shayiri kwa shekeli hamsini za fedha.
17 Akiweka shamba lake wakfu katika Mwaka wa Yubile, ile thamani iliyokwisha wekwa itakuwa hiyo hiyo.
18 Lakini akiliweka shamba lake wakfu baada ya Yubile, kuhani ataweka thamani kulingana na idadi ya miaka iliyobaki kufikia Mwaka wa Yubile unaofuata, na thamani yake iliyoamuliwa itapunguzwa.
19 Kama mtu anayeweka wakfu shamba anataka kulikomboa, lazima aongeze sehemu ya tano ya thamani yake, nalo shamba litakuwa lake tena.
20 Kama pengine halikomboi shamba hilo, au kama ameliuza kwa mtu mwingine, kamwe haliwezi kukombolewa.
21 Shamba hilo litakapoachiwa Mwaka wa Yubile, litakuwa takatifu, kama shamba lililotolewa kwa Mwenyezi Mungu, nalo litakuwa mali ya makuhani.
22 " 'Kama mtu ameweka wakfu kwa Mwenyezi Mungu shamba alilonunua, ambalo si sehemu ya

‡ **27:16** Homeri moja ni sawa na efa 10, ambazo ni sawa na kilo 100.

ardhi ya jamaa yake,
23 kuhani ataamua thamani yake hadi Mwaka wa Yubile, naye huyo mtu lazima alipe thamani yake siku hiyo kama kitu kitakatifu kwa Mwenyezi Mungu.
24 Katika Mwaka wa Yubile, shamba litarudishwa kwa mtu yule ambaye lilinunuliwa kutoka kwake, yule ambaye ardhi ilikuwa mali yake.
25 Kila thamani lazima iwekwe kulingana na shekeli ya mahali patakatifu§: gera ishirini kwa shekeli.
26 “ ‘Hata hivyo, hakuna mtu atakayemweka wakfu mzaliwa wa kwanza wa mnyama, kwa kuwa mzaliwa wa kwanza tayari ni mali ya Mwenyezi Mungu; awe ng’ombe au kondoo, ni wa Mwenyezi Mungu.
27 Kama ni mmoja wa wanyama walio najisi, aweza kumnunua kwa bei iliyowekwa, akiongeza sehemu ya tano ya thamani yake. Kama hatamkomboa, mnyama huyo atauzwa kwa bei iliyowekwa.
28 “ ‘Lakini chochote kile mtu alicho nacho na akakiweka wakfu* kwa Mwenyezi Mungu, iwe ni binadamu, au mnyama, au ardhi ya jamaa, hakiwezi kuuzwa au kukombolewa. Chochote kilichowekwa wakfu ni kitakatifu sana kwa Mwenyezi Mungu.
29 “ ‘Mtu yeyote aliyewekwa wakfu ili kuangamizwa, hawezi kukombolewa. Mtu kama huyo lazima auawe.

§ **27:25** Shekeli moja ya mahali patakatifu ni sawa na gramu 11.
* **27:28** *akakiweka wakfu* ina maana ya kumpa Mwenyezi Mungu kabisa, daima, bila kurudiwa.

30 “ ‘Zaka ya kila kitu kutoka shambani, iwe ni
nafaka kutoka kwa ardhi, au tunda kutoka kwa
miti, ni mali ya Mwenyezi Mungu; ni takatifu kwa
Mwenyezi Mungu.
31 Kama mtu akikomboa chochote cha zaka
yake, lazima aongeze sehemu ya tano ya thamani
yake.
32 Zaka yote ya kundi la ng’ombe au la kondoo
na mbuzi, kila mnyama wa kumi apitaye chini
ya fimbo ya yule awachungaye, atakuwa kitu
kitakatifu kwa Mwenyezi Mungu.
33 Yule mnyama wa kumi hatachaguliwa kwa
kigezo cha uzuri au ubaya, naye haruhusiwi
kubadiliwa. Akimbadili, basi mnyama yule
wa kwanza na huyo aliyebadiliwa wote wata-
hesabiwa kuwa watakatifu, na haiwezekani
kuwakomboa.’ ”
34 Haya ndio maagizo Mwenyezi Mungu aliy-
ompa Musa juu ya Mlima Sinai kwa ajili ya
Waisraeli.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025
72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d